

**Bongo** Fleva wamlilia JPM kwa nyimbo

UKURASA 20



**Mourinho** mambo magumu Spurs

UKURASA 21


## MAISHA

MACHI 21, 2021 Nipashe — Baba, Mama na Mwana — *Jumapili*



Ukurasa 10

**Mtajieni mtoto majina yenu na ya ukoo**



Ukurasa 15

**MAISHA NI NYUMBA**
Ubunifu muhimu kung'arisha kitanda



**HARUSI**

Ukurasa 12



**Vaa hivi msibani**

Ukurasa 13

UKURASA 9


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Machi 21, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0580526

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz  www.facebook.com/nipashetz  www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Simanzi, vilio

• **Samia** aongoza maelfu kuaga mwili wa JPM, Kikwete amlilia...*Ukurasa 2&3*




Rais na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Samia Suluhu Hassan, akiongoza viongozi na wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam, kuaga mwili wa aliyekuwa Rais, Hayati Dk. John Magufuli, katika Uwanja wa Uhuru, jana. **Picha zaidi Uk. 7. PICHA: OMR PICHA: YASMINE PROTUS**

## Wapinzani waweka matumaini kwa Samia

UKURASA 5

## Bagonza, Ruwa'ichi watoa kauli nzito kuhusu Magufuli

UKURASA 3 & 4




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play  App Store


**MICHEZO** MWAMBUSI KUREJESHA DOZI YANGA UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6



# Simanzi, vilio vyatawala kumuaga JPM



Baadhi ya wananchi wakiangua kilio katika viwanja vya Kanisa Katoliki, Parokia ya Mt. Petro Oysterbay, mkoani Dar es Salaam, wakati mwili wa Hayati Dk. John Magufuli ukifanyiwa ibada jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**.

**Na Waandishi Wetu**

SIMANZI na vilio vilitawala katika siku ya kwanza ya kuaga mwili wa Rais John Magufuli mkoani Dar es Salaam jana.

Hali hiyo ilishuhudiwa katika maeneo mbalimbali ulikopitishwa mwili huo kuanzia Hospitali ya Jeshi Lugalo hadi kwenye Uwanja wa Uhuru ambako viongozi wa kitaifa na wananchi waliuaga.

Mwili huo ulitoka Hospitali ya Lugalo majira ya asubuhi na kupitishwa Barabara ya Ali Hassan Mwinyi kupelekwa nyumbani kwake Ikulu na baadaye Kanisa Katoliki St. Peter lililoko Oysterbay ambako Rais Magufuli enzi za uhai wake alikuwa akisali huko na baadae uliondolewa kupelekwa Uwanja wa Uhuru.

Kwenye maeneo yote ambayo mwili huo ulipitishwa, simanzi, yowe na vilio vilitawala huku wananchi wakionyesha hisia zao kwa kumpa heshima maalum kwa kubeba matawi ya miti, mabango yenye ujumbe tofauti na baadhi ya wanawake wakinyoosha juu kanga na mitandio yao na wengine kuzitandika barabarani.

**SAFARI KWENDA UHURU**

Baada ya misa kanisani iliyoanza saa 2:13 asubuhi, mwili huo uliondolewa kanisani huko saa 3:10 asubuhi kwa msafara kuelekea Uwanja wa Uhuru ukipitishwa Barabara ya Uhuru, Ali Hassan Mwinyi, Morocco, Magomeni, Kigogo, Ilala Boma, Chang'ombe na hatimaye uwanjani huko.

Msafara wenye mwili wa Rais Magufuli ulipofika eneo la Mbuyuni katika Barabara ya Ali Hassan Mwinyi, wananchi wa maeneo hayo, maarufu kwa wauzaji wa maua, walionekana wakiyarusha maua barabarani na wengine wakitumia simu zao kupiga picha.

Katika Barabara ya Kawawa yenye mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka, baadhi ya wananchi walionekana wakiwa wamepanda juu ya daraja la mabasi hayo lililoko eneo la Morocco.

Wengine walijipanga kwa kusimama pembezoni mwa Barabara ya Kawawa inayoelekea Magomeni wakati wote mwili huo ukipitishwa kwa mwendo wa taratibu kuruhusu wananchi ambao wasingeweza kwenda Uwanja wa Uhuru siku hiyo, kutoa heshima zao za mwisho.

Mwaka 2017, Rais Magufuli alizindua barabara za mabasi yaendayo haraka ndani ya mkoa huo ambazo ni miongoni mwa miradi iliyotekelezwa wakati wa uhai wake.

Wanawake walishindwa kuzuia hisia zao kwa kutandaza kanga, maua na wanaume wakavua mashati na fulana kama ishara ya kutoa heshima zao za mwisho na kutambua mchango wa Rais Magufuli alioutoa kwao kwa kipindi cha miaka mitano na miezi minne kabla ya umauti kumkuta Jumatano ya wiki hii.

Kwenye maeneo mengine, baadhi ya wananchi walionekana wakipiga magoti wakati mwili wa Rais Magufuli ukipita ikiwa ni ishara ya heshima ya yale aliyoyafanya enzi za uhai wake kwa taifa, akigusa zaidi wananchi wanyonge aliojipambanua kwao.

Kadri mwili huo ulivyokuwa ukipitishwa katika barabara zilizotengwa, idadi ya wananchi nayo ilikuwa ikiongezeka.

Madereva wa bodaboda nao hawakubaki nyuma, walionekana wakipita katika barabara ya mabasi yaendayo haraka ya Kawawa huku wakipiga honi wakiusindikiza msafara huo.

**MACHINGA KARUME**

Msafara huo ulipofika Soko la Karume ambalo ni maarufu zaidi kwa nguo za mitumba mkoani Dar es Salaam, idadi ya waombolezaji iliongezeka zaidi na wengi wao wakiwa wametandaza barabarani nguo zao zikiwamo kanga kama ishara ya kumuaga Rais Magufuli.

Enzi za uhai wake, Rais Magufuli alikuwa mstari wa mbele kutetea haki za wanyonge na aliruhusu machinga kufanya biashara zao mahali popote bila kubughudhiwa na alijenga masoko na kutengeneza vitambulisho vya kuwatambua vinavyotolewa kwa gharama ya Sh. 20,000 kwa mwaka mzima.

Februari 25 mwaka huu, Rais Magufuli aliweka jiwe la msingi katika Soko la Kisutu ambalo litakapokamilika, litakuwa na uwezo wa kuhudumia wafanyabiashara 1,500 wakati awali lilihudumia 669.

Kitendo chake cha kuwajali watu wenye kipato cha chini, kimewagusa machinga na wananchi ambao jana wakati mwili wake ukipita Karume, wanawake walivua kanga na mitandio na kuingia katikati ya msafara na kuitandika barabarani huku vilio vikitawala wakati wote wa kupita kwa msafara huo.

Pia, walionekana baadhi ya wanaume wakiwa vifua wazi barabarani hapo wakitandika fulana na mashati yao kama ishara ya kumuaga mtetezi wao.

**ILIVYOKUWA KEKO**

Eneo la Keko, maarufu kwa wafanyabiashara wa samani, walimuaga Rais Magufuli kwa kumuimbia wimbo wa 'parapanda italia' huku wengine walibeba mabango yenye ujumbe unaosomeka "Kwa heri Jemedari Wetu", "R.I.P Chuma cha Wanyonge Tanzania".

Wengine walisikika wakisema "Magufuli ni mtu mwema", "Mungu amlaze mahali pema" na baadhi waliimba "baba... baba... baba.... hayupo ooh hayupo..." na kulia.

Kuna walioonekana wakiwa wamepanda kwenye paa za nyumba, magari ili kushuhudia msafara huo uliobeba mwili wa Rais Magufuli.

**UWANJA UHURU**

Baada ya mwili huo kufikishwa kwenye Uwanja wa Uhuru, vilio na mayowe vilisikika wakati wote wa kuushusha kuelekea eneo maalum lililotengwa kwa ajili ya misa na kuuaga.

Ulipowasili uwanjani huko, maofisa wa ngazi za juu wanane wa Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ), waliubeba huku majenerali wa jeshi hilo wakisindikiza pembeni kuupeleka eneo lililotengwa kwa ajili ya misa.

Mara baada ya mwili huo kuwekwa kwenye eneo maalum, Mama Janet Magufuli, akiwa amesindikizwa na wapambe wake, aliingia akilia na viongozi kadhaa ambazo sura zao zilionekana kujawa na simanzi.

Baada ya misa iliyoongozwa na Askofu Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Yuda Thaddeus Ruwa'ichi, kumalizika uwanjani huko, mwili huo uliwekwa eneo maalum ndipo Rais Samia Suluhu Hassan aliongoza shughuli ya kuaga na kufuatiwa na viongozi wengine wa kitaifa na kimataifa, viongozi wa dini, vyama vya siasa na baadaye walifuata wananchi.

Rais Magufuli aliagwa na makundi mbalimbali wakiwamo wanawake, wazee na watoto ambao walionekana walipofika mbele ya jeneza hilo wakiangua vilio na wengine wakisaidiwa na vyombo vya ulinzi na usalama baada ya kushindwa kutembea.

Shughuli za kuaga mwili huo siku hiyo ilitangazwa kuwa zilitarajia kuhitimishwa saa sita usiku na kwa wale ambao hawakupata nafasi hiyo mkoani humo, wataendelea leo.

**VIKAO CCM**

Katika hatua nyingine, Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu Taifa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ilikutana jana jijini Dar es Salaam, ambapo pamoja na mambo mengine, imeazimia kupendekeza jina la Rais Samia Suluhu Hassan kuwa Mwenyekiti wa chama hicho.

Akitangaza maazimio hayo jana, Katibu wa Itikadi na Uenezi wa chama hicho, Humphrey Polepole, alisema kamati hiyo pia imeazimia wanachama wao wajitokeze kwa wingi kuanzia leo hadi siku ya mwisho kuuaga mwili wa Rais Magufuli.

Polepole pia alisema chama hicho pia kimezungumza na serikali ili kuruhuru mwili wa Rais Magufuli kuagwa na wabunge bungeni jijini Dodoma kabla ya kupelekwa Uwanja wa Jamhuri.

***Imeandikwa na Romana Mallya na Hellen Mwango***





# Samia aongoza maelfu kuaga mwili

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameongoza maelfu ya wananchi na viongozi kuuaga mwili wa Rais John Magufuli kwenye Uwanja wa Uhuru wilayani Temeke mkoani Dar es Salaam.

Viongozi mbalimbali wa serikali kutoka Tanzania Bara na visiwani Zanzibar, viongozi wastaafu, wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), viongozi wa dini, ni miongoni walioshiriki kuuaga mwili huo katika siku ya kwanza ya shughuli hiyo jana.

Uagaji wa mwili huo kwa Dar es Salaam, ulipangwa kufanyika hadi saa sita usiku na utafanyika pia kwenye mikoa ya Dodoma, Mwanza, Geita na visiwani Zanzibar.

Baada ya misa iliyofanyika uwanjani huko jana ikiongozwa na Askofu Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Yuda Thaddeus, Ruwa'ichi, mwili wa Rais Magufuli ulipelekwa sehemu maalum iliyoandaliwa kwa ajili ya kutoa heshima za mwisho.

Shughuli za kutoa heshima za mwisho ziliongozwa na Rais Samia, aliyeaga na kuondoka uwanjani huko, akifuatwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah, na Mke wa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, Mama Maria Nyerere.

Wengine waliofuata ni mawaziri wakuu wastaafu ambao ni Joseph Warioba na John Malecela, wajumbe wa Kamati Kuu Taifa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Katibu Mkuu Kiongozi, Dk. Bashiru Ally, Spika wa Bunge mstaafu, Anne Makinda, Spika mstaafu wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Pandu Amiri Kificho na ndipo alifuata mjane Mama Janet Magufuli pamoja na familia yake.

Wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama walifuatia kutoa heshima za mwisho kwa Rais Magufuli na baadaye walifuata mawaziri na manaibu waziri na viongozi wengine ndani ya serikali kisha wananchi wakapewa nafasi.

Katika shughuli ya utoaji heshima za mwisho, makundi mbalimbali wakiwamo wanawake, watoto na wazee walionekana wakipita mbele ya jeneza lenye mwili wa Rais Magufuli huku baadhi yao wakishindwa kuficha hisia zao na kuangua kilio.

Vilevile, baadhi ya waombolezaji walianguka na kupata usaidizi wa askari wa vyombo vya ulinzi na usalama vinavyosimamia shughuli hiyo.



Askofu Mkuu wa Kanisa Katoliki, Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Yuda Thaddeus Ruwa'ichi, akiusalia mwili wa aliyekuwa Rais, Hayati Dk. John Magufuli, katika Uwanja wa Uhuru, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**.

# Ruwa'ichi: JPM alikuwa mtu wa haki

**Na Romana Mallya**

ASKOFU Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Yuda Thaddeus Ruwa'ichi, amesema Rais John Magufuli alikuwa mtu wa imani na haki na alimpa Mungu yaliyompasa na kuwataka Watanzania wamwombee Rais mpya, Samia Suluhu Hassan, kwa kuwa kazi ya urais siyo rahisi.

Kiongozi huyo wa kiroho aliyasema hayo jana alipoongoza misa maalum iliyofanyika kwenye Uwanja wa Uhuru mkoani Dar es Salaam na baadaye maelfu ya wananchi wakiongozwa na Rais Samia waliuaga mwili wa Rais Magufuli ikiwa ni siku ya kwanza ya shughuli hiyo.

Misa hiyo ilishuhudiwa pia na Katibu Mkuu wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Padri Charles Kitima, na aliyekuwa Askofu Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Kardinali Polycarp Pengo.

Katika misa hiyo, Askofu Ruwa'ichi alisema Rais Magufuli alilipenda taifa na kulihudumia kwa nguvu zake zote kusudi liendelee kuwa na umoja, amani huku akijituma katika kushughulikia ustawi wa maendeleo ya raia wake wote.

Alisema Rais Magufuli alimpa Mungu yaliyompasa na kutaka wakati wanamwombea, waliombee pia taifa ambalo alilipenda na kulihudumia kwa nguvu zake zote.

Alisema taifa limeingia kwenye safari ya maadhimisho ya msiba mzito wa kuondokewa na Rais Magufuli.

"Tuko kwenye majonzi, tuko kwenye maombolezo. Hata hivyo, tunapoomboleza, tutiwe nguvu na imani yetu katika Kristo ambaye Mheshimiwa Magufuli alimwamini, alimfuata, alimshuhudia na kumtumikia.

"Ninawaalika tunapokuwa kwenye majonzi, tufarijiwe na kutiwa nguvu na neno la Mungu. Somo la kwanza la leo (jana) linahusu hekima ya Suleimani, tumesikia kwamba roho za wenye haki zimo mikononi mwa Mungu. Tujiulize hivi mtu mwenye haki ni mtu wa namna gani?

""Mtu mwenye haki au wa haki ni yule ambaye yupo tayari kuwapa wengine stahili zao na kuhusu stahili, yapo mambo ni stahili ya Mungu kutoka kwa mwanadamu kiumbe wake. Tunapaswa kumwamini, kumwabudu na kumtumikia Mungu kwa imani safi na thabiti.

"Mtu wa haki anayo mambo ambayo anapaswa kuwatunukia binadamu wengine kama kuwapenda, kuwahurumia, kuwasaidia, kushikamana nao katika utendaji na majukumu ya maisha," alisema.

Askofu Ruwa'ichi aliendelea kuhubiri: "Mtu mwenye haki, anayo majukumu ambayo anapaswa kuyatekeleza kumhusu yeye mwenyewe, yaani kwa nafsi yake kama vile kujitunza, kujiheshimu, kuwajibika, na mambo kama hayo."

Alisema Hayati Magufuli alikuwa mtu wa imani na haki, alimpa Mungu yaliyompasa kama kiumbe wake na wenye stahili zao na akajipa mwenye stahili yake kama kiumbe wa Mungu.

Alisema wanayo kila sababu ya kumwombea ili Mungu amsamehe chochote kilichopungua katika kujitolea, uwajibikaji na utendaji wake wote ili amjalie pumziko la milele.

Ujumbe wa Askofu Ruwa'ichi kwa Watanzania ni kumwombea mrithi wa Rais Magufuli, Rais Samia aliyeapishwa juzi jijini Dar es Salaam kwa mujibu wa Katiba.

"Kuwa Rais wa nchi siyo kazi rahisi, ni jukumu zito ambalo linambebesha wajibu wa kuwahudumia kwa usawa raia wote. Ninajua kwamba Mama Samia alishirikiana kwa karibu na Rais Magufuli wakati akiwa makamu wake.

"Kwa hiyo, hatuna wasiwasi kwamba anaielewa nchi, anaifahamu nchi, anajua vipaumbele vyake, atayaendeleza kwa juhudi yale yote mema ambayo yalishughulikiwa na Magufuli.

"Kwa kuwa nimesema jukumu la kuongoza nchi ni jukumu zito, ninawaalika tumweke katika sala, tumpe ushirikiano na kushikamana naye katika kutafuta ustawi na maendeleo kwa kila raia wa nchi," alisema.

Askofu Ruwa'ichi alitoa pole kwa mjane wa Rais Magufuli, Mama Janeti Magufuli na familia na kuwatakia moyo mkuu kwa kusukumwa na imani wanapopita katika kipindi hiki.

"Tutiwe moyo na neno la Mungu kwani tunaamini kwamba Kristo aliyekufa na kufufuka pia ni tumaini letu la ufufuko," alisema.

## JK amlilia Magufuli

**Na Enock Charles**

RAIS mstaafu wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete, ameeleza masikitiko yake kufuatia kifo cha Rais John Magufuli kilichotokea Jumatano mkoani Dar es Salaam, akigusia kushtushwa na mazingira ya kifo chake.

Katika taarifa yake ya jana kuhusu msiba huo wa kitaifa, Kikweke, maarufu JK, alisema ameshtushwa na kifo hicho kwa maelezo kuwa hapakuwa na dalili zozote zilizoashiria kumpoteza kiongozi huyo wa juu serikalini hasa kutokana na mazingira ya kifo chake cha ghafla.

Kikwete aliyekuwa Rais wa Tanzania kuanzia mwaka 2005 hadi 2015, alieleza namna alivyopata tabu kuandika, lakini akiwataka Watanzania kumpa ushirikiano Rais mpya, Samia Suluhu Hassan.

"Tupeane pole Watanzania kwa msiba mkubwa uliotukuta, ni pigo kubwa, tena ni kubwa lisilomithilika. Rais wetu mpendwa Magufuli ametutoka ghafla bila kutazamia. 'I never saw this coming' (sikulitarajia hili kutokea).

"John Pombe Joseph Magufuli ametutoka wakati ambapo uongozi wake ulikuwa unahitajika sana, tulikuwa tunamhitaji kukamilisha aliyoyaanza na kufanya mazuri mengi aliyokuwa amepanga kuifanyia nchi yetu na sisi wananchi wake," alisema.

Kikwete alisema ana imani nchi ipo salama kwa kuwa Rais Samia anajua yaliyofanyika, yanayotakiwa kukamilishwa na yaliyopangwa kufanyika miaka mitano ijayo.

Alisema wengi wanatamani Magufuli angeendelea kuwa Rais na miaka mingi ijayo, lakini mapenzi ya Mungu hayawezi kubadilika.

Juzi, Rais Samia aliapishwa kuwa kiongozi mkuu wa nchi baada ya kifo cha Dk. Magufuli kilichotokea Jumatano katika Hospitali ya Mzena mkoani Dar es Salaam alikokuwa akipatiwa matibabu ya maradhi ya moyo.

"Wajibu wetu ni kumwombea kwa mola ampe pumziko. Daima tutamkumbuka Magufuli kwa mema mengi aliyoifanyia nchi yetu. Hakika Tanzania imepoteza kiongozi mzalendo wa dhati, shupavu, mahiri na makini," Kikwete alisema.

Alisema ana imani na mrithi wake, Rais Samia aliyekuwa Makamu wa Rais chini ya uongozi wa Dk. Magufuli hadi umauti ulipomkuta na kwamba anajua undani wa yale yaliyofanyika na yanayohitaji kukamilishwa katika kipindi cha miaka mitano.



## Vyama vya wafanyakazi: JPM tutamkumbuka hapa

**Na Mary Geofrey**

BAADHI ya vyama vya wafanyakazi, vimebainisha namna vitakavyomuenzi Rais John Magufuli, vikiwaomba viongozi wapya kutekeleza ahadi zake.

Vyama hivyo vimekumbusha kuwa wakati wa uhai wake, Dk. Magufuli alijitahidi kujali maslahi ya wafanyakazi bila kuwadanganya kuwaongeza mshahara.

Alinukuliwa akisema kuwa hakutaka kuwadanganya kwa kuwaongeza mishahara huku kwa upande wa pili wa shilingi serikali ipandishe bidhaa kama mafuta ya kula, sukari na zinginezo.

Akiwa katika mkutano wa kampeni katika Uwanja wa Mkendo, Musoma mkoani Mara Septemba 5, mwaka jana, Rais Magufuli alisema alijitahidi kuwajali watumishi na katika kipindi cha miaka yake mitano ya uongozi wake, alitoa ajira 61,000 zikiwamo za madaktari na walimu.

Rais Magufuli alisema kuwa wakati akiingia madarakani, alikuta watumishi hawajalipwa pensheni zao na kwa kipindi chake cha miaka mitano alilipa zaidi ya Sh. trilioni moja huku akilipa malimbikizo ya madeni ya watumishi zaidi ya Sh. bilioni 500.

### TUCTA WANAVYOMKUMBUKA

Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA), limesema litakuwa sehemu ya kukumbuka mazuri yaliyofanywa na kiongozi huyo.

Rais wa TUCTA, Tumaini Nyamhokya, jana alibainisha mazuri hayo kuwa ni pamoja na namna Rais Magufuli alivyoshughulikia sakata la utoaji wa mafao nchini akiagiza kusitisha utekelezaji wa kikokotoo kipya ambacho kilikuwa kinaathiri kwa kiwango cha mafao ya uzeeni kwa wafanyakazi.

Alisema Rais Magufuli aliruhusu kutumika kikokotoo cha zamani ambacho kina manufaa kwa wafanyakazi wastaafu nchini.

Alisema watamkumbuka Rais Magufuli kwa kupunguza makato ya Kodi ya Lipa Kadri Unavyopata (PAYE) kutoka asilimia 11 mwaka 2016 hadi tisa mwaka 2020.

Nyamhokya anasema pia aliwarudisha kazini baadhi ya wafanyakazi wenye elimu ya darasa la saba waliokuwa wameondolewa kwenye utumishi wa umma.

Alisema Rais Magufuli pia aliongeza ushirikishwaji wa wafanyakazi sehemu za kazi kupitia utatu na mabaraza ya wafanyakazi sehemu za kazi.

"Rais Magufuli aliongeza ajira kupitia utekelezwaji wa sera ya viwanda, miradi mbalimbali ya kitaifa na miundombinu ya huduma za kijamii nchini," alisema.

Alisema Hayati Rais Magufuli alikuw nguzo katika shughuli za wafanyakazi nchini kwa kuzingatia nafasi yake aliyokuwa nayo kama mkuu wa nchi, utu ubinadamu aliouonyesha katika kushu ghulikia masuala mbalimbali yanayoh wafanyakazi.

"Alishakaa na sisi mara nyingi zaidi kuliko uongozi wote uliopita, alitusha na kututatulia matatizo yote tuliyoele alisema Nyamhokya.

Alisema Rais Magufuli ameacha som kubwa kwa Watanzania kutokana na uzalendo wake wa kuipenda nchi na kujali maslahi ya wanyonge wakiwam wafanyakazi.

Alisema kuwa licha ya kuwa hakuongeza mshahara wa watumishi, alisaidia kudhibiti mfumuko wa bei, hali iliyosababisha thamani ya fedha kuendelea kuwapo.

"Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi nchini linawaomba wafanyakazi wawe watulivu na kushiriki kikamilifu katika hatua zote za maombolezo na mazishi kote nchini," alisema.

Alisema Hayati Dk. Magufuli ameacha somo la uzalendo kwa Watanzania wote kwa kufundisha kupenda na kuthamini vya kwao.

"Rais Magufuli ameondoka, ameacha funzo kubwa kwetu, nikiwa kama Mtanzania, ninajivunia juhudi kubwa alizofanya za kuijenga nchi kwa sababu ya uzalendo wake," alisema Nyamhokya.

Katibu Mkuu wa TUCTA, Said Wamba, alisema Rais Magufuli alifanya kazi iliyoacha alama bila kuogopa mataifa mengine wanasema nini dhidi yake.

### AJIRA MADAKTARI

Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (TALGWU), Rashid Mtima, alisema wamepokea kwa mshtuko na masikitiko makubwa taarifa za kifo na watamkumbuka Rais Magufuli na kumuenzi.

Alisema TALGWU watamkumbuka kwa kurejesha wafanyakazi wa darasa la saba kupitia vikao vinane walivyoketi kujadili suala hilo.

Alisema wanafanya kazi katika serikali za mitaa nchini katika awamu yake wamenufaika na ujenzi wa barabara vijijini, umeme na ujenzi wa vituo vya afya na zahanati.

"Tutamkumbuka sana kwa sababu siyo tu, manufaa hayo bali alitoa ajira 1,000 za madaktari ambao kwa asilimia kubwa walikuwa wanachama wa TALGWU.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akitokwa na machozi wakati akitoa heshima za mwisho kwa mwili ya aliyekuwa Rais, Hayati Dk. John Magufuli, katika Uwanja wa Uhuru, mkoani Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mkewe Mary Majaliwa. **PICHA: OWM.**

# Bagonza asema uthubutu wa Magufuli haukuwa wa kawaida

**Na Beatrice Moses**

ASKOFU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Karagwe mkoani Kagera, Dk. Benson Bagonza, amesema Rais John Magufuli alikuwa na uthubutu wa hali ya juu ulioiwezesha nchi kupiga hatua kubwa kimaendeleo ndani ya muda mfupi.

Kiongozi huyo wa kiroho alitoa kauli hiyo juzi alipotafutwa na Nipashe kuzungumzia kifo cha Rais Magufuli na kile kinachotajwa kuwa kiongozi huyo wa nchi alitabiri kifo chake kutokana na kauli zake za hivi karibuni kabla ya kukutwa na umauti.

Askofu Bagonza alisema kazi ya urais ni ya hatari na ndiyo sababu kuu ya Rais Magufuli kuona uwezekano wa kufariki dunia kwake.

"Ni kawaida viongozi wakifa, watu wanaanza kutengeneza fikra tofauti zinazoweza kuwa zinazohusiana na imani au hali halisi, pia zinaweza kuwa za kisayansi.

"Kiongozi yeyote aliyekabidhiwa jukumu zito na anayepata fursa ya kuongea na Mungu kila wakati, anafunuliwa mambo. Ninaamini alionyeshwa mwisho wa maisha yake, ni jambo zuri kuonyeshwa mwisho wa maisha yako wewe mwenyewe kuliko wakionyeshwa watu wengine wa pembeni," alisema.

Askofu Bangoza, akizungumza atakavyomkumbuka Dk. Magufuli, alisema "alikuwa na uthubutu wa hali ya juu sana ambao uliwezesha kuleta matokeo chanya japo kuna watu pia walijeruhiwa kutokana na uthubutu huo".

Kauli ya Rais Magufuli inayohusishwa na kutabiri kifo chake ni ile anayosisitiza Watanzania watamkumbuka kwa mazuri aliyokuwa anaifanyia nchi katika utendaji wake wa kazi.

"Siku moja mtanikumbuka, na mimi ninajua mtanikumbuka kwa mazuri na siyo kwa mabaya kwa sababu. Nimejitolea maisha yangu kwa ajili ya Watanzania maskini," Dk. Magufuli alisema katika moja ya hotuba zake.

Siku hiyo, Dk, Magufuli alitumia fursa hiyo kuwataka wananchi kusimama pamoja na kuacha kubaguana kwa vyama, dini makabali ili kui tuijenge Tanzania.

"Kufa tutakufa tu, unaweza kufa kwa malaria, ukafa kwa kansa, ukafa kwa magonjwa mengine kwa sababu kufa kupo, lakini kamwe usimwache Mungu, huo ndiyo wito wangu, tusimame na Mungu."

Kauli zingine za Rais Magufuli za kukumbukwa na zinaonekana kama alikuwa anatabiri kifo chake, ni aliposema:

"Ninataka Watanzania muamini mna Rais wa kweli kweli, jiwe kweli kweli, sitishwi wala sitishiki. Mimi jukumu langu kwa ajili ya Watanzania ni kuhakikiha ninawavusha Watanzania kutoka mahali pa shida wanaenda mahali pa raha, ninajua hiyo ndiyo itakuwa sadaka yangu kwa Watanzania.

"Ili kusudi hata nikienda huko mbinguni, siku moja Mungu atakaponihitaji, akanichague 'wewe ulikuwa kiongozi mzuri, unaweza hata kuwaongoza malaika polepole'.

"Inawezekana kuelewa ni kugumu na inawezekana itachukua muda lakini baadaye siku moja watakumbuka na mimi hilo nina uhakika. Mara nyingi Watanzani wana tabia ya kukumbuka ukishakufa, watakwambia pengo lake halitazibika."

Sheikh Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Alhad Mussa Salum, akiungumzia kuhusu suala hilo la kujitabiri kifo, alisema katika imani ya dini ya Kiislamu hujulikana kama Ilham.

"Kuna vitu ambavyo Mwenyezi Mungu anaweza kumwonyesha mja wake akawa anapata dalili au ishara ya mambo fulani juu ya mwisho wa maisha yake. Hii siyo watu wote wanapewa. Rais Magufuli alikuwa ni mtu ambaye anamuogopa Mwenyezi Mungu





Rais Samia Suluhu Hassan, akijadiliana jambo na Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemedi Suleiman, katika hafla ya kuaga mwili wa aliyekuwa Rais, Hayati Dk. John Magufuli, katika Uwanja wa Uhuru, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: OMR**

# Wapinzani waweka matumaini kwa Samia

**Na Waandishi Wetu**

VYAMA vya upinzani vimeeleza matumaini yao kwa Rais Samia Suluhu Hassan kuwa atakuza na kuimarisha demokrasia na kuwaunganisha Watanzania kuwa wamoja.

Viongozi wa vyama hivyo walieleza hayo kwa nyakati tofauti juzi na jana walipokuwa wakitoa maoni yao kutokana na hotuba yake fupi aliyoitoa juzi baada ya kula kiapo kuongoza nchi.

Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimesema licha ya kuwa na imani na Rais Samia Suluhu Hassan kuhusu hatma ya nchi kwa sasa, kitaeleza nini afanye kuwafuta wananchi machozi.

Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, baada ya kuhudhuria shughuli za kuuaga mwili wa aliyekuwa Rais wa Tanzania, John Magufuli, katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam jana, alisema Rais Samia anapaswa kufungua ukurasa mpya na hasa uwanja wa maridhiano ya kitaifa.

"Kwa sasa tumeitikia wito wa kuwafuta wafiwa machozi, baada ya maziko tutaeleza nini afanye (Samia) kuwafuta wananchi machozi, zaidi ya kushikamana kwenye msiba, ni vyema mshikamano huo ukamhusisha Rais.

"Baada ya maziko ni vyema akakutana na vyama vya siasa kupata mwelekeo wa pamoja wa namna ya kusonga mbele na kurekebisha makosa yakiwamo ya uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba 25, mwaka jana," alisema.

Katika andiko lake, Mnyika alisema Rais mpya anapaswa kufungua ukurasa mpya kwa kuwa hotuba yake ya juzi, imetoa zaidi mwongozo kuhusu mazishi na maombolezo.

Alisisitiza kuwa kwa sasa CHADEMA inasubiri hotuba yake itakayotoa mwelekeo kwa nchi baada ya maziko.

"Katika hatua hiyo atapaswa kueleza hatua atakazochukua kufungua ukurasa mpya katika uongozi wa nchi, kwa kuwezesha maridhiano ya kitaifa, kuhuisha mchakato wa kupata katiba ya wananchi, kurejesha haki za kidemokrasia na kujikita katika maendeleo ya watu.

"Katika hatua hiyo, rejea ya makosa ya nyuma yatakuwa ni mafunzo katika kuandika historia mpya kwa ukweli, umoja, haki na uwajibikaji," alisisitiza.

Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba, alimtaka Rais Samia kuanza kutekeleza majukumu yake kwa kutibu majeraha ya demokrasia na katiba mpya ili kuwaunganisha Watanzania.

Prof. Lipumba alisema chama chake kina matumaini makubwa na serikali mpya ya Samia, kwa kuwa alikuwa Makamu Mwenyekiti wa Bunge la Katiba, wakati wa mchakato wa katiba mpya.

"Chama chetu kina imani kubwa na Samia ambaye ni mwanamke wa kwanza kuongoza nchi yetu na serikali mpya juu ya kupata katiba mpya na kuwaunganisha Watanzania kuwa kitu kimoja," alisema

Alishauri kuwa ni vyema Samia akapata ushauri kutoka kwa viongozi ambao walikuwapo wakati wa mchakato huo wa kuandika katiba mpya.

"Uzuri yeye mwenyewe (Samia) alikuwa ni kiongozi wa mchakato huo. Pia wapo wengine kama Jaji Joseph Warioba na Profesa Palamagamba Kabudi. Hao watamsaidia sana katika suala la katiba," alisema.

Kaimu Mwenyekiti wa Chama cha ACT Wazalendo Taifa, Dorothy Semu, licha ya kumpongeza na kumtaka Rais Samia kuliunganisha taifa, alisisitiza kuwa chama hicho kinaamini atakuwa kiongozi wa mfano, ambaye ataliongoza taifa kwa upendo.

Pia alisema imani waliyo nayo ACT Wazalendo kwa Rais Samia ni kuona anaiongoza nchi bila kuweka kando misingi ya katiba, sheria na utawala bora.

"(Lakini) yatakwenda sambamba na kushamirisha yale mema yaliyofanywa na mtangulizi wake (Magufuli) na kurekebisha pale palipo na upungufu ili kwa pamoja tuweze kusonga mbele na kujiletea maendeleo.

"Sisi ACT wazalendo tumefurahi sawa na hotuba ya mama Samia Suluhu Hassan aliyoitoa leo (juzi) baada ya kula kiapo chake," alisema na kuongeza:

"Tumeipokea hotuba yake kwa uzito wa kipekee pamoja na rai yake kwa vyama vya upinzani na Watanzania kuwa tushikamane, tufutane machozi, tusahau yaliyopita."

**UMOJA VYAMA WANENA**

Pia Umoja wa Vyama vya Siasa Mkoa wa Arusha, wamemwomba Rais Samia kusimamia yale yote yaliachwa na Rais Magufuli ili kumuenzi na kuipeleka nchi katika nafasi nyingine ya kiuchumi.

Katibu wa Chama cha Demokrasia Makini Mkoa wa Arusha, Simon Ngilisho, alisema Rais Samia anatakiwa kufuata nyayo za mtangulizi wake, Magufuli, ambaye wakati wa uhai wake, alikuwa mtu anayejali nchi yake, kiboko ya mabepari na mpigania haki za wanyonge.

Alisema Magufuli alifanya mengi katika uongozi wake, hivyo yale aliyoyaacha ni vizuri Rais Samia akayaendeleza kwa kuwa ni mama shujaa, anayejua wananchi wanahitaji nini.

"Tutampa ushirikiano wa kutosha mama Samia na tunamuombea Waziri Mkuu Kassim Majaliwa mola ampe nguvu zaidi katika kipindi hiki kigumu, lakini pia tunaamini kuwa Waziri Majaliwa ataendelea na uchapaji kazi wake makini katika kuleta maendeleo ya taifa," alisema.

Naye Katibu Mwenezi wa Tanzania Labour Party (TLP) Mkoa wa Arusha, Geofrey Stephen, alisema chama chake kitamuunga mkono Rais Samia kwa kuwa tangu awali walijenga imani kubwa kwa serikali.

Mwenyekiti wa Chama cha Sauti ya Umma (SAU) Mkoa wa Arusha, Simon Bayo, alisema wamempoteza kiongozi shujaa wa Afrika mwenye uthubutu katika kufanya uamuzi mgumu na alitoa pole nyingi kwa Rais Samia, Watanzania, viongozi mbalimbali wa dini, serikali na kusisitiza zaidi amani, mshikamano udumu zaidi.

***Imeandikwa na Godfrey Mushi, Allan Isaack na Tumaini Mafie (ARUSHA) na Boniface Gideon (TANGA)**

# CHADEMA wasitisha uchaguzi

**Na Enock Charles**

BARAZA la Wanawake la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAWACHA), limesitisha kwa muda shughuli za uchaguzi wake kufuatia kifo cha Rais John Magufuli.

Katika taarifa ya baraza hilo kwa umma iliyotolewa jana, lilibainisha kuwa tayari chama hicho kupitia kwa Mwenyekiti wake, Freeman Mbowe, kimetuma salamu za rambirambi kwa mjane Mama Janeth Magufuli, mama mzazi wa Dk. Magufuli, Suzana Magufuli na Rais mpya Samia Suluhu na kwa Watanzania wote.

"Kufuatia msiba huu, tunasitisha kwa muda mchakato wa uchaguzi ikiwamo vikao vya uchujaji na uteuzi wa wagombea walioomba kujaza nafasi zilizotangazwa ndani ya baraza mpaka baada ya kipindi cha maombolezo," taarifa ya baraza hilo ilibainisha.

Ratiba ya kuaga mwili wa Raia Magufuli inaonyesha leo wanamalizia wakazi wa Dar es Salaam kwenye Uwanja wa Uhuru, kesho utakuwa Dodoma na keshokutwa utapelekwa Zanzibar na baadaye Machi 24 wananchi wa Mwanza kuaga kisha kusafirishwa kwenda Chato ambako utaagwa Machi 25 na kuzikwa Machi 26.

Uchukuaji na urejeshaji fomu za kuwania nafasi za uongozi BAWACHA ulifungwa Jumatatu, wagombea watatu wakijitokeza kuwania nafasi ya Kaimu Mwenyekiti, watano nafasi ya Kaimu Makamu Mwenyekiti Bara, saba kwa nafasi ya Katibu Mkuu, sita nafasi ya Naibu Katibu Mkuu Bara na mmoja kwa nafasi ya Naibu Katibu Mkuu Zanzibar.

Uchaguzi huo unafanyika kutokana na kitendo cha Novemba 24, mwaka jana cha makada wapatao 20 wakiongozwa na aliyekuwa Mwenyekiti wa BAWACHA, Halima Mdee, kwenda bungeni jijini Dodoma kuapishwa kuchukua nafasi 19 za ubunge wa viti maalum kinyume cha msimamo wa chama hicho kilichopinga matokeo ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka jana na kukubaliana kutokubali nafasi zozote zilizotokana na uchaguzi huo.

Mbali na Mdee, wengine waliofukuzwa ni pamoja na aliyekuwa Makamu Mwenyekiti wa Baraza hilo Bara, Hawa Mwaifunga, Katibu Mkuu Grace Tendega, Naibu Katibu Mkuu Bara Jesca Kishoa, Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, Asia Mohamed, Katibu Mwenezi, Agnesta Lambert, Katibu Mkuu wa Baraza la Vijana, Nusrat Hanje, na aliyekuwa Mwenyekiti wa Chadema Kanda ya Serengeti, Ester Matiko.

Wengine ni Cecilia Pareso, Tunza Malapa, Ester Bulaya, Felister Njau, Sophia Mwakagenda, Ngahenjwa Kaboyoka, Kunti Majala, Anatropia Theonest, Conchesta Rwamlaza, Salome Makamba na Stella Fiao.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kauli ya Rais iwe chachu katika kuwaunganisha Watanzania

**SAMIA** Suluhu Hassan, juzi alikula kiapo cha kuongoza Tanzania huku akitoa kauli thabiti iliyoonyesha kuwa ni mwanga wa enzi mpya yenye matumaini, upendo, amani na mshikamano kwa Watanzania wote bila kujali tofauti zozote walizonazo.

Mwanasiasa huyo, ambaye kabla ya kula kiapo hicho alikuwa Makamu wa Rais tangu mwaka 2015, anachukua nafasi ya John Magufuli aliyefariki dunia Jumatano wiki hii mkoani Dar es Salaam alikokuwa akipatiwa matibabu ya maradhi ya moyo.

Katika hotuba yake fupi aliyoitoa muda mfupi baada ya kuapishwa, Samia alitoa kauli nzito iliyoakisi dira ya mahali tuendako pale aliposema hakiharibiki kitu. Kwa hakika kauli hiyo iliwatoa hofu wale waliokuwa wameonyesha kukata tamaa kutokana na kifo cha Rais.

Hofu hiyo na dalili za kukata tamaa zilitokana na taharuki iliyoikumba nchi kwa kuwa tukio la Rais kupoteza maisha akiwa madarakani ni la mara ya kwanza tangu kuasisiwa kwa taifa la Tanzania mwaka 1964 pamoja na Uhuru wa Tanganyika mwaka 1961.

Rais Samia, katika hotuba yake hiyo, aliwahakikishia Watanzania kuwa wako imara kama taifa na viongozi wamejipanga vizuri kuhakikisha wanaendelea pale mtangulizi wake alipoishia huku akitanabahisha kwamba Magufuli alikuwa kiongozi asiyechoka kufundisha, kuelekeza kwa vitendo anavyotaka nchi iwe na anachotaka kifanyike. Hakuishia hapo tu bali alisema mtangulizi wake huyo alimlea na kumwandaa kwa majukumu mazito zaidi.

Pamoja na kuweka bayana hayo, Samia aliwataka Watanzania kuwa na moyo wa subira, kuvumiliana na kujenga umoja na mshikamano katika kipindi hiki ambacho Tanzania inapita katika wakati mgumu wa kuondokewa na kiongozi wake wa juu kabisa.


Ni wazi kwamba tangu kumalizika kwa uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 na serikali ya awamu ya tano kuingia madarakani, kumekuwa na manung'uniko kutoka kwa baadhi ya vyama vya siasa kwamba serikali imeminya demokrasia na uhuru wa vyombo vya habari.

Lakini matumaini yanaonekana baada ya Rais Samia kueleza kuwa Watanzania wasahau yaliyopita bali waungane kufarijiana, kuonyeshana upendo badala ya kuendelea kutengana na kuhasimiana.

Kwa wachambuzi wa masuala ya kisiasa na kijamii, haikuwa lazima kwa Rais kuweka kila kitu hadharani bali kauli yake imeonyesha kwamba liko jambo ambalo anataka kuwaeleza Watanzania kuwa kuna nafasi ya kuganga majeraha na kuzika tofauti ambazo kwa namna mbalimbali zimesababisha mpasuko miongoni mwa Watanzania.

Ni imani yetu kwamba mambo hayo yatawezekana ndiyo maana aliahidi kuwa atatafuta wasaa wa kuzungumza, kukumbushana na kuwekana sawa juu ya mambo mengi yanayohusu taifa, mustakabali wake na matarajio ya Tanzania chini ya uongozi wake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Tumuenzi Magufuli tukihimiza amani na kumtanguliza Mungu

**WATANZANIA** wamepata pigo kubwa kwa kuondokewa na Rais wa Serikali ya Awamu ya tano, Dk. John Magufuli, aliyefariki dunia Machi 17, jijini Dar es Salaam.

Dk. Magufuli amefariki dunia ikiwa ni zaidi ya miezi minne tu tangu aanze muhula wake wa pili wa miaka mitano baada ya uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba 28, mwaka jana.

Kifo chake kimewaacha na majonzi mengi watu wa kada mbalimbali wakiwamo wamachinga, ambao wanadai kwamba, hawajui hatima yao, kwa madai kwamba, mtetezi wao ameondoka.

Wanasema Magufuli alikuwa kimbilio lao kwa kuwa kila walipoona kuna watu wanataka kuwasumbua, katika maeneo yao ya biashara walikimbilia kwake na kuwasikiliza na kutatua kero zao.

Kwa maana hiyo, kifo chake ni pigo kubwa kwao, kwa kuwa wanaamini kwamba, sasa watakosa mtetezi aliyehakikisha wanafanya biashara eneo lolote bila kusumbuliwa na mtu au kiongozi yeyote.

Lakini nikirejea kwenye hoja yangu, katika uongozi wake, yako mengi ambayo amelifanyia taifa hili kwa ajili ya maendeleo, ambayo kila mmoja wetu hana budi kuyaendeleza.

Msisitizo wake katika kujiletelea maendeleo, ulikuwa katika kulinda amani, mshikamano, kufanya kazi kwa bidii na kujitegemea bila kubaguana kwa mrengo wa dini, kabila wala siasa.

Hayo ni kati ya mambo ambayo enzi ya uhai wake alikuwa akisisitiza katika hotuba zake na kuweka wazi kuwa serikali itafanya kila lililo ndani ya uwezo wake kulinda amani, utulivu na mshikamano wa Watanzania.

Bila amani na utulivu, nchi haiwezi kuendelea na badala yake ni vurugu na mgawanyiko miongoni mwa Watanzania, ndiyo maana alisisitiza kila Mtanzania kulinda amani kwa nguvu zote.

Tangu nchi ipate uhuru, amani, umoja na mshikamano miongoni mwa mambo ambayo Watanzania wanaendelea kujivunia, kwa kuwa vina mchango katika maendeleo ya nchi.

Hatua yake ya kuhimiza hayo, ilionyesha kwamba kulikuwa na watu waliokuwa na lengo la kuitaharisha, hivyo akaona kuna haja ya kuhimiza amani katika kila hotuba zake.

Wakati huu ambao tunaendelea kuomboleza, hatuna budi kukumbuka na kuhimizana kila mmoja kuendelea kulinda na kudumisha amani kama ambavyo alikuwa akihimiza.

Msiba huu mkubwa usaidie kuwaunganisha Watanzania, kwa kutambua kuwa hata mwenyewe alikuwa akitamani watu wasikubali kugawanywa kwa misingi ya dini wala vyama bali wazingatie umoja wa kama Watanzania.

Ni jukumu la kizazi cha sasa kuendeleza na kulinda yote mema yaliyoasisiwa na kusimamiwa na taifa hili ambayo Magufuli katika hotuba zake, neno amani halikukosekana kinywani mwake.

Hiyo inatokana na ukweli kwamba, amani na usalama, umoja, mshikamano wa kitaifa, moyo wa kujitolewa na kujitegemea ni miongoni mwa nyenzo muhimu ya kufikia lengo la kuwa na taifa lenye maendeleo endelevu.

Ulinzi wa amani si chaguo, ni wajibu ambao kila mtu katika jamii anapaswa kuuvaa, kwa kuwa bila amani jamii husambatarika, hivyo ni vyema kila Mtanzania kutimiza wajibu wake kulinda amani iliyopo.

Ikumbukwe kuwa hakuna mtu ambaye anaweza kwenda katika shughuli za uzalishaji mali ama sehemu yoyote kama nchi haina amani, hivyo tumuenzi Rais Magufuli kwa kuendelea kulinda amani uliopo.

Siku chache kabla ya kifo chake aliyekuwa Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan (sasa Rais) alikaririwa na vyombo vya habari akisema, huu ni wakati wa Watanzania kushikamana, kwa maana ya kuwa wamoja.

Umoja wetu kama Watanzania ambao umekuwapo kwa miaka yote uimarike zaidi hasa wakati huu wa msiba mkubwa ili hatimaye tuvuke salama ili maisha yaendelee.

Magufuli pia alikuwa akitukumbusha kuwa maendeleo hayana chama, hivyo kila mmoja bila kujali chama chake, ashiriki katika shughuli mbalimbali za maendeleo kwa ajili ya nchi yake.

Lakini kikubwa zaidi katika msisitizo wake, ilikuwa ni kila mmoja kwa dini yake, kumtanguliza Mungu kwa kila jambo kwa kuwa ndiye muweza wa yote.



# HAYATI JPM AAGWA DAR ES SALAAM



Wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama, wakiwa kwenye ibada ya kuuombea mwili wa Hayati Dk. John Magufuli, katika Kanisa Katoliki la Mt. Petro Oysterbay, mkoani Dar es Salaam jana. Kutoka kushoto ni Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Venance Mabeyo, Mkuu wa Jeshi la Polisi, Simon Sirro, Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa, Diwani Athuman, Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza, Suleiman Mzee, Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dk. Anna Makakala, Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, John Masunga na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Brigedia Jenerali John Mbungo. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Maofisa wa Jeshi la Ulinzi wa Wananchi Tanzani (JWTZ), wakilitoa nje jeneza lenye mwili wa aliyekuwa Rais, Hayati Dk. John Magufuli, baada ya kumalizika kwa ibada katika Kanisa Katoliki Parokia ya Mtakatifu Petro Oysterbay. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Umati wa wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, wakiwa kando ya Barabara ya Kawawa, wakiangalia msafara wa magari uliokuwa umebeba jeneza lenye mwili wa Hayati Dk. John Magufuli ukielekea katika Uwanja wa Uhuru. **PICHA: ANTHONY SIAME**



Familia ya Hayati Dk. John Pombe Magufuli, wakati wa kuaga katika Uwanja wa Uhuru. **PICHA: OMR**




Waombolezaji wakiaga mwili wa Hayati Dk. John Magufuli, katika Uwanja wa Uhuru. **PICHA: JUMANNE JUMA**




Mmoja wa waombolezaji akiangua kilio, wakati wa kuaga katika Uwanja wa Uhuru. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## KONA YA UKWELI

# Kwa heri JPM, asante kwa kusafisha ufisadi



Na Thobias Mwanakatwe

MACHI 17, 2021 saa 5:00 usiku hakika itabaki kuwa siku ya kihistoria kwa Watanzaia. Ilikuwa siku ambayo wananchi tulipewa taarifa mbaya na za kuumiza mioyo yetu.

Taarifa hizo zilitolewa na aliyekuwa Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, ambaye sasa ni rais baada ya kuapishwa juzi, zilihusu kifo cha Rais wetu mpendwa, Dk. John Magufuli.

Kiukweli hii ni taarifa mbaya kabisa kuwahi kutokea katika ardhi ya Tanzania kufiwa na Rais akiwa madarakani. Lakini huu ndio ukweli kwamba Magufuli hatunaye tena.

Vyombo vya habari, yaani redio, televisheni na mitandao ya kijamii vilianza kutangaza taarifa za kifo cha Magufuli, hivyo kuongeza majonzi makubwa kwa Watanzania. Nilikuwa nikifuatilia vyombo vya habari jinsi vilivyokuwa vikihoji wananchi ni namna gani watamkumbuka Dk. Magufuli katika utawala wake wa zaidi ya miaka mitano.

Hakika ni mambo mengi ya kukumbukwa na ambayo viongozi wanaobaki wanapaswa kuyaenzi. Mengi yaliyozungumzwa na wananchi ni pamoja na Magufuli alivyothubutu kutoa elimu bure kwa wanafunzi jambo ambalo alilisimamia kwa mafanikio makubwa.

Mengine ni vitambulisho vya wajasiriamali ambavyo viliwawezesha wafanyabiashara wadogo maarufu kama wamachinga kuweza kufanya biashara zao kwa uhuru zaidi bila kunyanyaswa tofauti na ilivyokuwa awali ambapo wamachinga walikuwa paka na panya na mgambo wa jiji na miji.

Suala la maboresho ya afya kwa kujenga zahanati kila kijiji na kituo cha afya kila kata ni jambo la muhimu ambalo Magufuli atakumbukwa na Watanzania wengi pamoja na suala la uboreshaji wa miundombinu ya barabara.

Uthubutu wake katika kutenda mambo kwa manufaa ya Watanzania kuliwafanya wananchi wa nchi zingine za Afrika wamtamani angekuwa rais kwenye nchi zao. Hakika tumepoteza jembe, jemedari ambaye historia yake kamwe haitafutika.

Kwangu mimi kitu kikubwa ambacho nitamkumbuka Magufuli alivyopambana na ufisadi nchini ambao ulifikia hali mbaya sana ambapo baadhi ya watumishi ndani na nje ya serikali kwao suala hili lilikuwa jambo la kawaida na kulihalalalisha rasmi.

Utendakazi na jitihada za kupambana na ufisadi za Magufuli zimeifanya Tanzania ishike nafasi ya kwanza barani Afrika katika vita dhidi ya ufisadi.

Ripoti ya utafiti uliofanywa na mashirika ya Transparency International (TI) na Afro- Barometer ilisema Tanzania imeibuka ya kwanza barani Afrika katika kategoria mbili za kupambana na ufisadi na rushwa.

Asilimia 50 ya Watanzania walioshirikishwa kwenye utafiti huo, wanaamini kuwa licha ya kuweko vizingiti vingi katika vita dhidi ya ufisadi, lakini aghalabu ya wananchi wako tayari kuchukua hatua za kupambana na ufisadi wa kifedha.

Watu 47,000 walishirikishwa kwenye utafiti huo uliofanyika kati ya Septemba 2017 and Septemba mwaka 2018 katika nchi 35 za bara Afrika. Magufuli katika enzi za uhai wake alitamani wakati nitakapomaliza muda wangu wa uongozi, Tanzania iwe na mabilionea zaidi ya 100.

Ripoti hiyo ilionyesha kuwa, Tanzania imeipiku Rwanda katika kupambana na ufisadi, kwani mwaka 2018 Rwanda ilishika nafasi ya kwanza kwa alama 56, ikifuatiwa na Tanzania pointi 36, Uganda (26), Burundi (17) na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (19).

Kimsingi, inaumiza sana kuondokewa na kiongozi mwenye maono kama Magufuli, lakini ambacho nasisitiza sana kwa Watanzania ni kuwa waangalifu wala tusikubali kuharibu umoja wetu.

Tuendelee kushikamana zaidi huku tukijua kwamba ni sisi Watanzania ambao tunapaswa kupambana kwa kadri tunavyoweza kuendelea kuifanya nchi yetu kuwa bora kwa kila kitu. Ni sisi Watanzania ambao tunapaswa kufanya kila linalowezekana kuhakikisha amani yetu inaendelea kuwapo.

Mara kadhaa, Magufuli alikuwa akisisitiza tusifikiri tunapendwa sana na wenzetu walioko nje ya nchi, wakiwamo majirani zetu.

Huo ndio ukweli. Ni wajibu wetu Watanzania kulifahamu hilo. Ni wajibu wetu kushikamana kama Watanzania na kuona kwamba kinachoweza kutusaidia kuvuka hata kwenye kipindi hiki kigumu ni kushikamana.

Shime Watanzania, tushikamane zaidi na zaidi, tuache maneno au matendo yoyote ya kutugawanya. Yeyote anayetoa lugha za kutugawa, chukua hatua haraka ikiwamo kuripoti katika vyombo vya dola ili sheria ziweze kuchukua mkondo wake.

Fahamu kwamba hakuna lililo la msingi katika maisha yetu kama AMANI, ni lazima tuilinde kwa hekima na nguvu zote... Ndipo mengine yoyote ya maendeleo yanaweza kuja. Dk. Magufuli kwa kheri baba... Pumzika kwa AMANI!

## DARASA LA NDOA

# Namna ya Kutawala Msongo wa Mawazo - 2



Na Mch. Dk. Enock Mlyuka

KATIKA sehemu ya kwanza ya makala hii, tulijifunza maana ya msongo wa mawazo, visababishi vyake na athari zitokanazo na msongo wa mawazo kwa mwanadamu.

Sehemu hii ya pili inajaribu kuainisha ni nini kifanyike ili kutawala msongo wa mawazo? Ni jinsi gani unaweza kuzuia, kupunguza au kuondoa msongo wa mawazo? Inawezekana ziko njia nyingi za kukabiliana na msongo wa mawazo lakini hapa kuna baadhi ya njia za msingi na muhimu;-

**Kumshirikisha Mungu**

Kuna baadhi ya mambo katika maisha yetu hayamalizwi kwa vikao, bali mpaka Mungu aingilie kati. Hivyo, usitegemee akili zako tu. Jizoeze kumweleza Mungu mambo yako ili upate kupewa haki yako.

**Kutenda kwa juhudi na maarifa**

Watu wengi wanafanya kazi nyingi na kubwa kwa nguvu bila maarifa. Matokeo yake, kazi hiyo inawapatia tija kidogo na mara nyingine inawapa hasara zaidi. Kiini cha kukosa faida na mafanikio inawezekana ikawa ni kukosa maarifa. Maarifa yanayostahili kwa kila kazi yanaweza kukufanya ufanye kazi ndogo, yenye ufanisi wa kiwango cha juu kisha ukakusanya faida au mafanikio makubwa.

**Uwe na malengo ya maisha**

Kuishi bila malengo na kusudi husababisha maisha yasiyo na mwelekeo. Ni muhimu uwe na lengo na kusudi la maisha yako. Mfano, jiulize je, unataka kuwa nani? Unataka kufika wapi? Lini na kwa namna gani? Baada ya kipindi au muda gani? Na kwa nini unataka kuwa hivyo?

Usifanye mambo kwa kutaka kuiga wengine wakati huna uwezo. Kumbuka ule usemi wa Kiswahili usemao, "Usifuate kujisaidia kwa tembo utapasuka msamba." Fanya mambo ambayo una uwezo nayo.

**Kula chakula bora**

Mtu akiwa na msongo wa mawazo, anahitaji kula vizuri kwani mwili unakuwa umepoteza nguvu na vitamini nyingi. Wataalam wa afya hawashauri kutumia vileo wakati mtu akiwa na msongo wa mawazo kwani hudhoofisha afya ya mwili. Hivyo, mtu anashauriwa kula chakula bora. Wakati unapokula chakula, usiwe unakumbuka habari za kazi zako au matatizo yako.

**Toa madukuduku yako**

Usitunze matatizo na kubeba watu wanaokuumiza moyoni. Sema. Usiposema, iko siku yatakuua. Tafuta msaada wa kusikilizwa na kupata ushauri nasaha. Pata mtu mwaminifu mwenye uwezo na hekima; mwenye nia ya kukusikiliza na kutunza siri.

Wanasaikolojia wanasema, "Problem shared, half solved." Kumbuka unapozungumza na kushirikisha tatizo, unapunguza msongo na machungu nafsini mwako. Kataa kuwa mtu wa vinyongo na kuweka mambo moyoni kwani huko ni kujimaliza mwenyewe pole pole. Kutokuweka matatizo moyoni kunaongeza siku za kuishi za mtu.

**Watembelee wanaokufanya upate furaha**

Jichanganye na watu lakini angalizo hapa ni kwamba, angalia usichanganmane na watu wenye tabia au lengo la kukupotosha na kuongeza msongo zaidi. Umakini unahitajika katika eneo hili. Changamana na watu watakaosababisha amani na furaha nafsini mwako.

**Mazoea ya kucheka**

Kucheka ni fursa ya pekee ambayo binadamu amepewa na Mwenyezi Mungu. Kisaikolojia, kucheka hupunguza msongo wa mawazo na maumivu ya nafsi.

Kicheko huleta uponyaji. Huzuia magonjwa ya moyo; huongeza siku za kuishi; hutufanya tuwavutie wengine; hutusogeza karibu na wengine na kutufanya tufikike; huboresha uhusiano; na hupunguza hasira. Zaidi sana, kucheka huongeza hali ya kujiamini, humpa mtu nguvu mpya; huchochea ubunifu; huleta furaha na hupunguza uwezekano wa kuzeeka haraka.

Mwanasaikolojia William James anasema: "We don't laugh because we are happy. We are happy because we laugh." Maana yake ni kwamba hatucheki kwa sababu tuna furaha, bali tunafuraha kwa sababu tunacheka.

Kwa hiyo, cheka ili ufurahi na kuongeza siku zako za kuishi hapa duniani. Pale unapoona kucheka ni tatizo kwako, basi jitahidi kukaa na watu ambao watakufanya ucheke au ufurahi mara kwa mara.

**Penda kufanya mazoezi**

Mazoezi yanajenga mwili na kuimarisha afya zetu; yanaondoa sumu mwilini pia. Jenga tabia ya kupenda mazoezi kama vile kutembea, kukimbia, na kuendesha baiskeli.

Wataalamu wanasema mazoezi mazuri ni yale yanayochukua dakika 30 na yasiyozidi dakika 60. Fanya mazoezi mepesi mepesi yakihusisha mwili mzima. Yasiwe mazoezi ya kutumia nguvu sana. Fanya mazoezi ya wastani kwa kuyafurahia. Unapofanya mazoezi usifikiri matatizo, ubongo unahitaji kustarehe pia. Mazoezi huburudisha na kuondoa misononeko.

**Fanya matembezi**

Usijifungie ndani, fanya matembezi pia badilisha mazingira. Chukua hatua ya kutoka na kwenda katika mazingira mengine ambayo ni salama ili kuburudisha akili na nafsi.

**Tafuta sababu**

Ukijua sababu zifanyie kazi, kwani kujitambua ni sehemu ya suluhu ya matatizo ya mtu.

Itaendelea Jumapili Ijayo

■ ***Dk. Mlyuka ni Mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maoni, mafunzo na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au WhatsApp +255655865555.***

MAISHA
MACHI 21, 2021
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili



Ukurasa 10

## Mtajieni mtoto majina yenu na ya ukoo



Ukurasa 15

**MAISHA NI NYUMBA**

## Ubunifu muhimu kung'arisha kitanda



## HARUSI

Ukurasa 12



# Vaa hivi msibani

Ukurasa 13

Ukurasa 14

# Mtajieni mtoto majina yenu na ya ukoo

**Na Moses Ismail**

NI mtoto wa miaka sita hivi, anajua kuzungumza na kujieleza kwa baadhi ya mambo yanayofanana na umri wake, kwa maana hiyo unategemea ukimuuliza "baba yako anaitwa nani?" itakujibu; "Anaitwa Salehe."

Lakini badala yake utashangazwa na jibu lake, kama jina lake ni Juma, atakujibu: "anaitwa baba Juma." Vivyo hivyo, ukimuuliza; "na mama yako anaitwa nani?" Atakujibu: "Anaitwa mama Juma."

Hii inatokea kwa watoto wengi wa umri huo wanaopotea, unapowauliza maswali kama hayo ili kupata mahali pa kuanza kuwapa msaada, inakuwa vigumu kwao kutaja majina ya wazazi wao. Hawayajua.



Utajiuliza, inakuwaje mtoto huyu hafahamu majina ya wazazi wake? Kwa nini anawaita 'baba fulani' na 'mama fulani' kama anavyosikia watu wanavyowaita?

Achana na mtoto huyo, iwapo wewe una umri wa miaka 30 na kuendelea, jiulize ni lini ulianza kujua majina ya wazazi wako hasa mama yako? Lini ulijua ulifahamu kuwa mama yako anaitwa Amina?

"Daaah! Nilianza kulijua jina la mama yangu nikiwa 'fomu wani' hivi. Ila la baba nililijua mapema kwa vile ndilo lililokuwa likiandikwa kwenye nyaraka zote za majina yangu " Anajibu Julius Baitu, mkazi wa jijini Dar es Salaam.

Baitu, 46, anasema: "Haikuwa rahisi kulijua jina la mama yangu kwa sababu sikuwahi kusikia mtu akimuita kwa jina lake, nilikuwa nasikia anaitwa 'mama Neema' tu kwa sababu dada yangu wa kwanza anaitwa Neema."

Na ingawa hili ni jambo linalowahusu watoto, lakini lipo zaidi kwa watu wa Tanzania Bara tofauti na wenzao wa Zanzibar. Kwa maana ya Zanzibar watoto hiyajua majina ya mama zao wakiwa wadogo tu.

Jaribu kumuuliza Makame ama Usi au Haji; "Mama yako anaitwa nani?" Atakujibu; "anaitwa Bi. Mariam" Analijua jina la mama yake kama ilivyo la baba yake.

Kwa Zanzibar mtoto hulijua jina la mama yake utotoni, tangu akiwa licha ya kusikia mama yake akiitwa 'mama yake Usi' au 'Mama yake Raya', pia huwasikia akimwita kwa jina lake pia liwe 'Bi. Mariam' au jina jingine lolote.

Hata katika masomo yao, hasa ya dini, mtoto hutakiwa ajue majina ya wazazi wake wote wawili ili apate kijitambua vizuri kama ilivyo kwa baadhi ya shule za kisasa za 'intaneshino' zinavyofundisha hivi sasa.

Kwa wakumbatia mila na desturi, huenda hili la mtoto kujua jina la mama yake akiwa bado mdogo si jambo zuri na linakiuka utamaduni. Unaweza kukubaliana nao hivyo.

Lakini je, ni lipi lilolo bora, ni vyema mtoto akafahamu majina ya wazazi wake wote wawili na ikawa rahisi kwa watu wengine kumsaidia pindi anapopotea hasa katika kipindi hiki cha utandawazi au ni bora kulinda desturi ya kumficha jina la baba na mama yake?

## NA HAMIS KIDAGO 0657 207168 QUIZ

Weka maneno yafuatayo katika mtitiriko utakaoyafanya yalete maana kamili.

**Mfano: marguerite/est/La/fleur/une** →La marguerite estune fleur.

oiseau/Le/un/est/perroquet

Le perroquetest un oiseau.

plantesfragiles/Les/rosiers/des/sont

Les rosierssont des plantesfragiles.

un/saumon/poisson//est/Le

Le saumonest un poisson.

est/erable/arbre/un/L'

L'erableest un arbre.

citron/est/Le/fruit/un

Le citron est un fruit.

poireau/un/est/Le/légume

Le poireauest un légume.

des/Le chien et le chat/animauxdomestiques/sont

Le chienet le chat sont des animauxdomestiques.

bambou/une/Le/est/herbe

Le bambouestuneherbe.

qui/méne au success/est/Le/un/pont/fragile

Le pont qui méne au success est un pont fragile.

c'est/l'histoire/qui commence/Entre/au hazard/nous

Entre nous c'estl'histoire qui commence au hazard.

d'avoir/Sois/raison/et puis/sûr/vas-y

Soissûrd'avoir raison etpuis vas – y.

la durée/le soleil/de la nuit/apparaîtra/Quelquesoit

Quelquesoit la durée de la nuit le soleilapparaîtra.

Jibu kama kwenye huo mfano hapo chini.

**Mfano: Tu as une valise?** – Oui, j'aiune valise de mon frère.

Vousavez des chaussures de marche? – Oui, j'ai des chaussures de monpère.

Tu as un appareil photo? – Oui, j'aiunappareil photo de moncopain.

Vousavezunetente de camping? – Oui, j'aiunetente de mon cousin.

Tu as unevoiture? Oui, j'aiunevoiture de mes parents.

Tu as des skis? – Oui, j'ai des skis de ma sœur.

Vousavezun sac à dos? Oui, j'aiunsac à dos de ma tante.


Tu as unstylo? Oui, j'aiunstylo de monvoisin.

Vousavezuneboisson à consommer? Oui, j'aiuneboisson de ma petite amie.

Tu as des lunettes? Oui, j'ai des lunettes de monami.

## WATOTO

## PAKA RANGI







Alichokifanya daktari

MWALIMU aliingia darasani na kuwauliza wanafunzi juu ya ndoto zao za baadae.

**Mwalimu:** John we unataka ukiwa mkubwa uwe nani?

**John:** Nataka niwe daktari wa moyo niwasaidie Watanzania wanaougua magonjwa ya moyo.

**Mwalimu:** Vizuri, wewe Rose unataka kuwa nani?

**Rose:** Nataka kuwa rubani, niweze kusaidia watu wanaopenda kusafiri kwa anga.

**Mwalimu:** Safi sana Rose. Utakua mfano kwa wasichana wenzio kuwa na bidii kwenye masomo ya sayansi.

**Mwalimu:** Na wewe Nehemiah ??

**Jeremia:** Mimi nataka kuwa tajiri mkubwa sana. Niwe na nyumba Tanzania, Afrika Kusini na Dubai.

**Mwalimu:** Ndoto nzuri sana lakini unahitaji bidii sana kutimiza. Haya na wewe Juma unataka kuwa nani??

**Juma:** Nataka kuwa mlinzi wa Jeremia kulinda mali zake

**SWALI**
Rais wa kwanza Tanzania anaitwa nani?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Michepuko inavyotesa ndoa nyingi

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee kujuzana masuala mbalimbali ya maisha yalivyo katika familia na jamii yetu kwa jumla. Mitikisiko, mipasuko, mafarakano, talaka na mengineyo ni sehemu ya maisha yetu kila uchao. Na kila nyumba kuna aina ya kituko kinachorindima ndani yake.

Leo tujadili ndoa zilizobarikiwa mwanzoni lakini zinaishia vibaya baada ya kuvamiwa na nguvu toka nje ya ndoa. Sababu kubwa ikiwa ni mmoja wa wanandoa amekiuka kiapo cha ndoa na kuanzisha familia nyingine.

Hebu tusikie kilio cha mama mmoja anayetaabika baada ya mumewe aliyejitosa kwa mchepuko na kuanzisha familia nyingine inayomtesa.

Mama mmoja akanipigia simu hivi majuzi akinieleza yale anayopitia katika ndoa yake. Tayari amestaafu miaka minne iliyopita lakini hana amani wala raha kutokana na purukushani anazokumbana nazo.

Akasema hivi, "mimi ni mke wa ndoa, mama wa watoto wawili, wa kiume na wa kike. Tulifunga ndoa nzuri na mume wangu, maisha yalikuwa mazuri kwani tulikuwa na uchumi mzuri.

Hata hivyo baada ya kitambo nikaja kugundua kwamba mume wangu alikuwa na mwanamke mwingine kabla yangu ambaye ana watoto naye wawili. Hilo hakuniambia, nikavumilia kwani nami nilikuwa tayari nimeshazaa watoto.

Kana kwamba hiyo haitoshi, tukiwa ndani ya ndoa akazaa tena mtoto na mwanamke mwingine. Nilipopata habari nikamuuliza akawa mkali. Bila aibu, ili kuniumiza zaidi akawa anawaleta hao watoto wake wa nje nyumbani kwangu.

Ikafikia wakati akaondoka nyumbani kwangu na kuhamia huko kwa michepuko yake ambako alikaa kwa zaidi ya miaka 10 hadi aliporejea hivi karibuni. Watoto hao wa nje wamekuwa wakinitishia maisha kila wakati pasipo sababu."

Msomaji wangu, kuna vituko vingine ukisimuliwa utadhani ni ndoto kumbe ni kweli. Kwa kifupi, tatizo kubwa lipo kwa mwanamume huyo ambaye anateswa na roho mbili, zinaa na ile ya mitala.

Zinaa ni roho kuu inayowashambulia wanadamu. Ni silaha hatari iliyoachiliwa na majeshi ya kuzimu kuangamiza wanadamu. Zinaa pia ni dhambi mbaya kwa sababu inafanyika ndani ya mwili. Kumbuka miili yetu ni hekalu la Mungu. Kuruhusu zinaa unamhuzunisha Mungu.

Madhara makuu ya zinaa ni pamoja na kukuondolea ujasiri na pia heshima, inasababisha magonjwa sugu kama UKIMWI. Inakuondolea uwepo wa Mungu na pia inafungua milango ya majini mahaba kukumiliki.

Kingine kinachomtesa baba huyo ni roho ya mitala. Hii inahusika kusababisha ndoa za wake wengi, kuolewa au au kuoa wanawake tofauti. Kuoa na kuacha au kuachwa.

Roho hii inasababisha kukosekana kwa upendo kati ya wanandoa, kutofurahia ndoa, ugomvi usioisha baina ya wanandoa. Imesababisha hatma ya watu wengi kuharibika na ni chanzo cha ndoa nyingi kuvunjika. Imefanya watu kuoa na kuacha matokeo yake watu wanakuwa wajane katika umri mdogo.

Msomaji wangu, hizo ndizo roho ninazoona kumtesa baba huyo. Mkewe amekuwa mvumilivu pamoja na vituko vyote hivyo anavyofanyiwa na mumewe pamoja na watoto wa michepuko.

Mara nyingi nimezungumza kupitia safu hii kwamba kabla mtu hajaoa au kuolewa, atulie na kutafakari. Je, anamtaka mwenza wa aina gani? Pia amuombe Mungu umfunulie kuhusu yule anayemtaka.

Watu wengi wanakurupuka wanapokutana ama na mwanamume au mwanamke. Unakutana na mtu ana gari, nyumba au kazi nzuri, haraka haraka unamkubalia kuoana. Hujui kama ana mtu mwingine, tena aliyezaa naye. Wewe unajitosa mnafunga ndoa. Matokeo yake unajua baadaye.

Kuingia kwenye uhusiano kunahitaji utulivu na uvumilivu mwingi. Mshirikishe pia Mungu akupe maelekezo. Mungu anaongea nasi kupitia matukio mbalimbali. Anaweza kukutahadhari kupitia meseji za mwenzio kupitia simu yake. Hapo akikutaarifu kuwa wewe hauko peke yako, yupo mwingine anayemfuatilia mpenzi wako. Sauti yaweza kukujia kabisa kuwa 'huyo hakufai', lakini ukapuuza.

Wapo watu baada ya kujua kuwa walikosea au kuharibu, hutumia ubabe kuficha uovu wao. Unajua ulimuacha mke miaka kadhaa, badala ya kuomba msamaha unakuwa mkali. Yatupasa kumuomba Mungu sana atupe neema ya uvumilivu na mwisho mwema usio na karaha. Maisha Ndivyo Yalivyo.

***Niishie hapa msomaji tukutane tena wiki ijayo. Je, una maoni, kisa cha maisha? Nitumie kwa ujumbe kupitia 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Tumuenzi Magufuli kwa vitendo iwe kumbukumbu yenye kung'ara

NCHI imegubikwa na majonzi ya kuondokewa na Rais Dk. John Magufuli. Hii ni mara ya kwanza kwa kiongozi mkuu aliyeko madarakani kufariki dunia.

Magufuli anakumbukwa kwa kurejesha nidhamu na uwajibikaji serikalini, utekelezaji wa miradi ya maendeleo kama miundombinu ambayo imerahisisha usafiri na kuunganisha maeneo mbalimbali nchini.

Kutokana na miradi hiyo, mwonekano wa maeneo mengi umebadilika hasa kwenye barabara kutoka eneo moja hadi lingine. Sasa wakulima na wafanyabiashara wanasafirisha mazao na bidhaa kwa urahisi zaidi, hivyo kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Kwa Dar es Salaam, barabara za mitaa na kuu zimesaidia kupunguza na kumaliza kero ya foleni ambayo ilisababisha watu kupoteza muda mrefu barabarani badala ya kutumia muda huo kwenye uzalishaji.

Miradi mingine ni reli ya kisasa ambayo itarahisisha usafiri wa kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma, ambao kwa kiasi kikubwa itapunguza muda unaopotea kwa usafiri wa mabasi.

Mradi mwingine ni bwawa la kisasa la Mwalimu Nyerere ambalo likikamilika litazalisha umeme wa kutosha na ziada ambayo itauzwa kwa nchi zingine na kumaliza kero ya muda mrefu ya kukatika au kukosekana kwa umeme.

Rais Magufuli atakumbukwa zaidi kwa elimu bure ambayo wananchi wa kipato cha chini walisomesha watoto wao hadi sekondari bila kulipa ada na michango mingine ambayo ilikuwa kikwazo kwao.



Kwenye usafiri wa anga alisimamia kulifufua Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) na kuhakikisha kuna ndege mpya pamoja na miundombinu ya viwanja vya ndege pamoja na kujenga vipya.

Katika afya miradi mingi ilitekelezwa ambayo imesaidia kuboresha huduma za afya kwa ngazi ya zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya, rufani za mikoa, kanda na zile za kibingwa za kitaifa na wananchi kupata huduma husika kwa wakati na kwa haraka zaidi.

Kwenye miundombinu ya maji nako kuna mabadiliko makubwa ikiwamo kuhakikisha maji safi na salama yanapatikana, kwa kukabiliana na ubadhifu wa fedha za miradi huku kukiwa na miradi hewa mingi.

Kwa upande wa rushwa, aliongoza mapambano ya rushwa na kuchukua hatua kwa ambao walihusika kwa namna moja au nyingine, jambo ambalo liliweka Tanzania katika ramani ya dunia.

Sekta ya ardhi, wako waliodhulumiwa haki zao kwa miaka mingi, waliporwa ardhi, iliuzwa mara mbili hadi tatu, na kupewa wengine lakini chini ya uongozi wake watu walipata haki yao ya ardhi.

Chini ya uongozi wake hati zilitolewa kwa haraka na kwa wakati, jambo ambalo liliongeza thamani ya ardhi.

Kwa ujumla kwa kipindi cha miaka mitano na miezi minne aliyoongoza Tanzania imetekelezwa miradi inayoonekana na imeacha alama na ikiendelezwa lengo la kuboresha maisha ya watu, ni muhimu iendelezwe na kusimamiwa vizuri.

Ili kumuenzi vyema kiongozi huyo ni muhimu sana miradi iliyoanza ikakamilika, iliyofika nusu imaliziwe na iliyokamilika itunzwe ili isaidie vizazi na vizazi, katika kuhakikisha maisha malengo ya kuwa na miradi hiyo inatimia.

Ni muhimu sana maono ya Rais Magufuli kwenye maendeleo ya katunzwe na kuendelezwa, usimamizi wa uwajibikaji na nidhamu kwa watumishi wa umma ni muhimu mno katika kupambana na rushwa ili mwananchi wa kawaida kupata haki ya msingi.

Kwa nyakati hizi ile lugha ya unanijua mimi iliondoka kabisa na kila mmoja aliwajibika ipasavyo, na hakukuwa na rushwa kama ilivyokuwa kipindi cha nyuma, jambo ambalo linapaswa kuendelea kwamba iliyo haki ya mtu aipate na bila kutoa rushwa.

Ni muhimu serikali ya awamu ya sita ikasimamia na kuendeleza uwajibikaji na nidhamu serikalini, miradi ya maendeleo na mapambano dhidi ya rushwa ili kuhakikisha Tanzania inazidi kusonga mbele na kukuwa kiuchumi kutoka uchumi wa kati ya chini hadi uchumi wa kati.

Ikiwa usimamizi wa karibu utafanyika ikiwamo kupambana ipasavyo na rushwa, naamini miradi yote ya maendeleo itakamilika na wananchi wataona thamani ya kodi wanayotoa, wataona jinsi fedha zao zinatumika.

***Bwana ametoa, Bwana ametwaa jina lake lihimidiwe. Pumzika kwa Amani Rais wetu Dk. John Magufuli. Amina.***

# HARUSI



Je, upo katika matayarisho ya harusi yako hivi karibuni na unataka kupata picha mkiwa ufukweni? Basi angalia picha zifuatazo ambazo zitakupa mwanga wa namna ya kupiga picha katika eneo hilo.





MITINDO

# Vaa hivi msibani

KATIKA mila na desturi za Kiafrika watu hufarijiana pale inapotokea msiba kwa kujumuika pamoja na kupeana pole.

Katika hali hiyo hata aina ya mavazi huwa ni tofauti, mara nyingi huwa na nguo za kujisitiri kwa wanawake na wanaume.


Lakini kutokana na mabadiliko ya kijamii, watu wamebadilisha namna ya uvaaji, kutoka ule wa zamani wa kuvaa khanga kiunoni na ushungi kichwani hadi surualia, gauni na fulana.

Uvaaji huu wa kisasa unatokana na watu kugeukia tamaduni za nje na kuona nguo zenye rangi nyeusi ndio maalum katika misiba.

Wabunifu nao wanaongeza vionjo katika mavazi hayo ikiwa pamoja na kuweka picha za mtu aliyefariki pamoja na maandishi ya maombezo ili kumnogesha mvaaji.

Hata hivyo, unachoshauriwa utakapovaa nguo za aina hiyo lazima kuzingatia maadili ya kiafrika ikiwamo kuwa na ukubwa sahihi unaositiri na kutobana sana mwili.

Kama nguo za aina hiyo huna, basi unaweza kuvaa gauni la kitenge au dera, kasha ukatupia kilemba kichwani na kipande kimoja cha kitenge au khanga begani.









URBEMBO



# Mbinu rahisi kusafisha na kung'arisha miguu

KATIKA viungo vya binadamu ambavyo vinatumika sana, lakini vinapuuzwa katika usafi ni miguu.

Kwa kawaida miguu hutumika kama nyenzo muhimu ya kutoka sehemu moja hadi nyingine, bila viungo hivi inakuwa vigumu kufanya shughuli zako kwa ufanisi.

Miguu inapata suluba nyingi, lakini kwa bahati mbaya ni wachache wanaojua umuhimu wake na kuitunza vizuri.

Utunzaji wa miguu hauna gharama kubwa, ni kutumia akili zako katika kuhakikisha kiungo hiki muhimu kinakuwa safi.

Sasa kaa kwa umakini kusoma hapa ili kufahamu mbinu sahihi kusafisha miguu yako.

**OSHA KWA MAJI**

Wakati unaoga, hakikisha unatumia muda kiasi kuosha miguu, sugua katikati ya vidole kwa kutumia kitambaa kisafi.

Ili kuhakikisha unaosha vizuri, unatakiwa uiname kidogo wakati wa kuoga na kuosha kwa vidole vyako, kama huwezi tumia brashi maalumu Hakikisha baada ya kuoga, unakausha miguu yako vizuri ili kuepuka vijidudu vinavyosababisha fangasi.

**LOWEKA MIGUU**

Unaweza pia ukatumia mbinu ya kuloweka miguu kwa kutumia maji ya uvuguvugu.

Hakikisha maji yanakuwa na sabuni ya maji ambayo ni maalum kwa kulinda ngozi.Usitumie maji ya moto kabisa wakati wa kulowesha miguu. Ukimaliza pakaa mafuta aina yoyote kwa ajili ya kulainisha ngozi.

**ANIKA VIATU**

Hakikisha unaanika viatu baada ya kuvaa ili vikauke. Kufanya hivyo ni kwa ajili ya kuepuka unyevunyevu pamoja na vimele vya wadudu.

Kama una matatizo ya kunuka miguu loweka miguu yako kwenye mchanganyiko wa maji na siki.

**MATATIZO YA KIMAUMBILE**

Ujauzito, kisukari na kuzeeka unasababisha miguu kuharibika upesi na wanahitaji kuvaa viatu vyenye soli nzuri.

MAPISHI

Na Mary Geofrey



# Biriani ya nyama ya ng'ombe

**MAHITAJI**

NYAMA ya ng'ombe nusu kilo, mchele nusu kilo, vitunguu viwili, viazi mbatata viwili, vitunguu swaum saizi, tangawizi, curry powder, nyanya ya kopo kipakti kimoja na binzari nyembamba ya kusaga nusu kijiko.









Mahitaji mengine ni binzari manjano nusu kijiko cha chai, mafuta ya kupikia, chumvi (salt), rangi ya chakula, maziwa ya mgando kikombe kimoja cha chai, hiliki nzima, karafuu na amdalasini kiasi mti mmoja.

**MATAYARISHO**

Katakata nyama kisha ioshe na uiweke kwenye sufuria kisha tia kitunguu swaum, tangawizi, nyanya, curry powder, binzari zote, chumvi na maziwa ya mgando kisha bandika jikoni ichemke mpaka nyama iive na mchuzi ubakie kidogo.

Baada ya hapo kaanga viazi na uweke pembeni, kisha kaanga vitunguu na mafuta mpaka viwe vya brown na kisha uvitie viazi vitunguu, na mafuta yake katika nyama. Koroga na uache uchemke kidogo kisha ipua na utie fresh coriander iliyokatwa na hapo mchuzi wako utakuwa tayari.

Baada ya hapo loweka mchele wako kwa muda wa dakika 10, kisha chemsha maji yatie chumvi, hiliki, karafuu, pilipili mtama na abdalasin na mafuta.

Yakisha chemka tia mchele na uache uchemke mpaka ukauke maji yakisha kauka tia rangi ya chakula na uanze kugeuza ili ichanganyike na wali wote. Baada ya hapo ufunike na uache mpaka uive. Na baada ya hapo biriani litakuwa tayari kwa kuliwa.

# MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**

# Ubunifu muhimu kung'arisha kitanda



USAFI wa kitanda ni jambo muhimu ambalo linapaswa kufanywa kila siku katika nyumba.

Pia kufanywa muda wowote ndani ya siku hiyo moja kwa kutegemea matumizi yake ilimradi kionekane kisafi wakati wote. Msingi mkubwa wa usafi wa kitanda hiki ni lazima uanzie asubuhi unapoamka.

Na usafi ninaouzungumzia hapa ni kuanzia kutandika mashuka katika kitanda, kufuta vumbi katika pande zote zinazokizunguka na kukipangilia vizuri.

Shughuli hizo zote ili zifanikiwe kwa umakini na ustadi zaidi zinapaswa kufanyika muda mfupi baada ya kuamka na si vinginevyo.

Uzoefu unaonyesha kwamba mtu anapoamka na kuanza kutandika kitanda bila kuchelewa ama kufanya shuguli za nyumbani anaweza kufanya vizuri zaidi kuliko akisubiri kwanza afanye usafi wa kinywa.

Na hata kama akifanya anaweza asifanye kwa umakini ama ustadi zaidi kama inavyokuwa anapoamua kufanya hivyo muda mfupi baada ya kuamka.

Kwa sababu kitanda ni mojawapo ya vitu vinavyoifurahisha nafsi katika nyumba na kiafya pia, ni vizuri kikapewa kipaumbele kikubwa.

Ili nafsi yako ifurahi kweli na kukusaidia upendelee kuwapo nyumbani mwako kuburudisha macho, kuna umuhimu wa kuhakikisha unakitendea haki kitanda kwa kukifanyia usafi na kukitandika vizuri.

Kama nilivyosema, muda mzuri unaofaa kukifanyia usafi kitanda na kukitandika ni asubuhi baada ya kuamka japokuwa hata baadae endapo utakitumia utapaswa kukiweka sawa kama kitakuwa kimevurugika.

Kitu cha muhimu ni kuhakikisha unakuwa na shuka lako unalotumia kulalia pamoja na lile unalojifunika, ambalo utalitumia katika shughuli hiyo ya kutandika na endapo utaona inafaa zaidi kulingana na uwezo wako, unaweza kutenga shuka za kutumia katika kulalia na za kutandika pekee.

Pia kuna mbinu nyingi za kukifanya kitanda chako kiwe katika hali ya usafi na mvuto wa kipekee na uepuke kukiacha kichafu bila kutandika.

Kumbuka kila kitu kinahitaji ubunifu, jitahidi kuongeza ubunifu kila siku kutafuta namna bora ya kukifanya kitanda chako kipendeze kwa sababu lengo kubwa ni kupendezesha nyumba yako, nafsi na ustawi wa afya yako pia.





## MPANGILIO

# Dondoo wakati wa kuchagua viwanja kwa ajili ya ujenzi

**1:** Hakikisha eneo linafikika, uwepo wa barabara na upatikanaji wa mchanga au matofali.

**2:** Zingatia eneo kama halipo mabondeni, mbali na mto, mfereji au mkondo wa maji.


**3.** Eneo lisiwe karibu na viwanda kuepukana na athari za kimazingira.

**4.** Hakikisha unapata vibali kutoka mamlaka sahihi za nchi kwa kufuata taratibu.

**5.** Chagua eneo lenye upatikanaji wa huduma muhimu kama maji, usafiri, shule, maduka na masoko.



# KATUNI




*KINYUNYIZO CHA LEO...

...TUPANGUSE MACHOZI TUYAONE MEMA YAKE...

## HABARI KIMATAIFA

# Kenyatta azidi kumlilia Magufuli

**NAIROBI, Kenya**

RAIS wa Kenya, Uhuru Kenyatta, jana amekwenda ubalozi wa Tanzania nchini Kenya, kwa ajili ya kutia saini kitabu cha rambirambi kwa aliyekuwa Rais wa Tanzania, Hayati Dk. John Pombe Magufuli.

Rais Magufuli alifariki dunia Machi 17 kutokana na matatizo ya moyo jijini Dar es Salaam.

Kenyatta alikwenda katika ubalozi uliopo jijini Nairobi akiambatana na viongozi wakuu wa nchi hiyo, wakiwamo maspika wa mabunge mawili, Kaimu jaji wa Mahakama ya juu zaidi na mawaziri.

Baada ya tukio hilo Rais Kenyatta alisema "Tumekuja kuwahakikishia mshikamano wetu kwa Watanzania katika wakati huu mgumu. Tunataka mfikishe rambi rambi zetu binafsi na zile za Wakenya kwa Rais Samia Suluhu Hassan,".

"Tunamwombea. Tunataka mumhakikishie uungaji mkono wetu na kwamba kazi nzuri ya kaka yetu (Rais Magufuli) imeanza, tutaendelea nayo,"Rais Kenyatta alimwambia Balozi John Stephen Simbachawene ambaye alimpokea.

Viongozi wa mabunge hayo pia walitoa rambi rambi zao na kwa niaba ya wabunge wenzao waliowawakilisha.

Katika taarifa yake kuhusu kifo cha aliyekuwa rais wa Tanzania, aliyoitoa wiki hii, kiongozi huyo alimtaja Magufuli kama rafiki yake binafsi na kiongozi mwenzake.

BB



Mhamiaji kutoka Honduras, Dustin akiwa na mtoto wake wa miaka sita, Jerrardo, wakimulikwa na mwanga wa jua la asubuhi mara baada ya kuingia nchini Marekani kwa kuvuka mpaka na Mexico juzi. **(PICHA:REUTERS)**

# Umoja wa Ulaya kuanza tena kutoa chanjo ya AstraZeneca

NCHI za Umoja wa Ulaya zimeanza tena kutoa chanjo ya AstraZeneca baada ya kupokea hakikisho jipya juu ya usalama wa chanjo hiyo kutoka kwa shirika la udhibiti wa madawa la Umoja wa Ulaya (EMA).

Chanjo hiyo ilianza kutolewa tena katika majimbo kadhaa nchini Ujerumani, wakati Ufaransa Waziri Mkuu wake, Jean Castex alichomwa chanjo hiyo mbele ya waandishi wa habari.

Serikali za Umoja wa Ulaya zinajaribu kuongeza imani kwa umma kwamba chanjo hiyo ni salama baada ya matumizi yake kusitishwa mwishoni mwa wiki iliyopita, kutokana matatizo ya kuganda kwa damu kwa watu wachache walioipokea chanjo hiyo.

Chanjo ya Astrazeneca imeidhinishwa na Shirika la Afya Ulimwenguni WHO, pia ni moja kati ya chanjo nne za Covid-19 zilizoidhinishwa na Umoja wa Ulaya.

Zoezi la kutoa chanjo lilienda taratibu katika eneo hilo tangu lilipoanza mwishoni mwa mwezi Desemba, mwaka jana

DW.

=================

# Libya kuchunguza waliouawa Benghazi

**TRIPOL, Libya**

WAZIRI Mkuu mpya wa Libya, Abdulhamid Dbeibeh, amesema amempa maelekezo mwanasheria mkuu wa serikali ya taifa hilo kuanzisha uchunguzi huru baada ya kugundulika miili ya watu waliouawa.

Mapema siku ya Alhamisi, vyombo vya habari nchini humo vilisema miili ya watu kadhaa waliouawa kwa kupigwa risasi ilipatikana katika mji wa mashariki wa Benghazi, uliokuwa unadhibitiwa na wapiganaji wanaomuunga mkono Jenerali Khalifa Haftar.

Kiongozi hiyo ambaye alichaguliwa katika mchakato ulioongozwa na Umoja wa Mataifa, na kuanza kazi yake wiki hii aliandika katika ukurasa wake wa Twitter kwamba kitendo hicho hakiwezi kuvumiliwa na kufumbiwa macho.

DW

=================

# Maandamano yaendelea Myanmar

**NAY PYI TAW, Myanmar**

MAANDAMANO ya kupinga mapinduzi ya kijeshi nchini Myanmar yameendelea kupamba moto na jana watu walizidi kumwagika mitaani wakitaka kurudisha utawala wa kiraia.

Wakati maandamano hayo yakiendelea, jumuiya ya kimataifa inazidi kuushinikiza utawala wa kijeshi kusitisha ukandamizaji dhidi ya waandamanaji.

Nchi jirani za Asia zimejiunga na mataifa ya magharibi kulaani matumizi ya nguvu. Rais wa Indonesia Joko Widodo alisema ataiomba Brunei ambayo ni mwenyekiti wa Jumuiya ya nchi za kusini Mashariki mwa Asia (ASEAN) kuitisha mkutano wa dharura.

Usiku wa kuamkia jana watu wawili walipoteza maisha baada ya askari kufyatua risasi katika mji wa kaskazini wa Mogok. Hadi kufikia sasa idadi ya waliouwwa tangu yatokee mapinduzi Februari mosi mwaka huu, imefikia watu 237.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, jana alilaani kile alichokiita jeshi kuendelea na vurugu za kikatili

DW.

# Uturuki yajiondoa mkataba kulinda haki za wanawake

**ANKARA, Uturuki**

UTURUKI imejiondoa katika mkataba wa Ulaya unaowalinda wanawake dhidi ya ukatili.

Rais Recep Tayyip Erdogan, jana alitia saini amri ya kujiondoa katika mkataba wa Istanbul, na kuelezwa ni pigo kwa wanaharakati na watetezi wa haki za wanawake.

Walisema makubaliano hayo yalikuwa muhimu katika kupambana na unyanyasaji wa wanawake majumbani.

Kwa mujibu wa watetezi wa haki za binadamu, kumekuwa na ongezeko la ukatili na mauaji dhidi ya wanawake nchini humo.

Tangu mwaka huu uanze wanawake 77 wameuawa, kulingana na jukwaa linalofuatilia mauaji ya wanawake.

DW.

# Katikati ya kipindi kigumu lakini muhimu



Na Magabilo Masambu

TANGU kutangazwa kwa taarifa za kifo cha John Magufuli, Rais wa awamu ya tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Machi 17, mwaka huu, Watanzania kwa ujumla tumekuwa na kipindi kigumu sana. Ugumu wake unatokana na sababu mbalimbali. Moja, ni kwa sababu hii ni mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu Rais kufariki dunia akiwa madarakani. Sababu nyingine ni juu ya utendaji wake wa kazi kwa kipindi chake chote tangu akiwa waziri mpaka Rais.

Waswahili husema matatizo ni kipimo cha akili. Matatizo hasa makubwa yanapotokea huwa pia yanatumika kupima mambo mbalimbali kwa mwanadamu. Ustahimilivu, hekima na busara ni miongoni mwa mambo yanayopimwa na ukubwa wa tatizo katika uamuzi wakati wa tatizo lenyewe.

Jambo kama hili lilionekana mwaka 1999 wakati wa msiba wa Baba wa Taifa, Hayati Walimu Nyerere. Baada ya kifo chake, Watanzania wengi tulijawa na hofu iliyotokana na kuamini kwamba bila Baba wa Taifa kuwapo, taifa litayumba. Lakini busara na hekima za viongozi wetu zilitumika vyema na leo tupo tunadunda kama kawaida.

Hofu ni jambo la kawaida litokeapo jambo lolote ambalo si la kawaida. Hata sasa najua hofu ni kubwa. Wengine tunajiuliza itakuwaje, hili na lile litafanywaje, nani atakuwa nani na kadhalika. Lakini ndugu zangu Watanzania tujipe moyo, haya yote tukiwa na utulivu yatakwisha na tutavuka salama.

Kipindi hiki ni kigumu lakini muhimu kwa sababu ni kipindi kitakachoamua hatima ya nchi na uongozi wetu kwa ujumla. Ni wakati muhimu kwa mstakabali wa amani, umoja na mshikamano wetu kama taifa. Nikiri kwamba kwa miongo kadhaa tumekuwa wamoja na bado ni wamoja na hasa wananchi wa kawaida ukiachana na wanasiasa.

Lakini pia ni ukweli usiopingika kwamba umoja, upendo na mshikamano wetu kama taifa umetikiswa na tusipokubali hili waziwazi hatutalitatua. Mwalimu Nyerere amewahi kusema: "Hatuwezi kutatua matatizo yetu kwa kujifanya kwamba hayapo." Ili utibu tatizo lazima ukubali kwamba lipo, halafu unalitafutia tiba.

Njia bora kabisa ya kutatua matatizo na mogogoro tuliyo nayo ni mazungumzo. Kuna wakati unaweza kudhani jambo ni kubwa sana kiasi cha kutumia bunduki za kivita, kumbe lingeweza kumalizwa kwa njia ya mazungumzo na maisha ya kaendelea.

Ukweli wa kimungu ambao hautaweza kupingwa kwa namna yoyote ile, ni kwamba binadamu si mkamilifu. Binadamu yeyote lazima awe na pande mbili za shilingi. Atakuwa na mema na upande wa pili atakuwa na mabaya. JPM kwa kuwa ni binadamu kwa vyovyote vile, kuna mema amefanya na katika udhaifu ule ule wa kibinadamu, amefanya mabaya. Tukiwa binadamu ambao tunatenda pande mbili pia, tuchukue mema yake na tumsamehe katika mabaya yake.

Eneo moja kubwa na jema ambalo JPM amefanya kwenye uongozi wake. Napenda pia nimshauri Rais Samia Suluhu Hassan ashikilie hapo hapo kurudisha nidhamu ya watumishi wa Umma. Kwa hilo JPM hatasaulika nafahamu amefanya mengi, lakini hili ni muhimu zaidi kwa sababu ndilo linalomgusa mwananchi mmoja mmoja katika huduma za jamii. Iifika wakati ukihudumiwa unaulizwa kama umeridhika na huduma, tofauti na huko nyuma ambapo wananchi walionekana hawana maana na hakuna aliyejali.

Tunayo katiba ya nchi pamoja na ubovu wake tunapaswa kuiheshimu kwasababu ndiyo inayotuweka madarakani, tunaapa kuilinda. Pili, umuhimu wa haki za binadamu kama ulivyotamkwa katika katiba hiyo pamoja na mikataba ya kimataifa, uhuru wa watu kusema kwa mujibu wa katiba.

Kama ambavyo ibara ya 37 ya katiba ilivyofuatwa, basi hata nyinginezo zizingatiwe ili kuwa na maelewano ya pamoja. Eneo la mahakama pia lirudishe imani kwa wananchi kwamba haki zinapatikana huko.

Msiba huu utukumbushe sisi tuliobaki kujitafakari juu ya maisha yetu hapa duniani. Fedha, madaraka na vingine vyote tunaviacha hapa duniani. Kwa vyovyote vile ni vyema tuvitumie kustawisha maisha ya wengine na kama hatuwezi basi angalau tusiwaumize.

Mwisho, tumuunge mkono na tumtie moyo Rais. Ni ukweli kwamba hatakosa kasoro lakini ndiyo hukamilisha ubinadamu wake. Tujikite zaidi katika kumfanya atekeleze majukumu yake vizuri, kutokubalika kwa kila mtu hiyo ni kawaida hata Yesu pamoja na kuwaponya watu, bado walimsulubu.

***0689157789***
***magabilomjalifu@gmail.com***
***ARUSHA-TANZANIA***

# Wavulana mashineni, wasichana kutwanga, vinginevyo walala njaa



Na Adam Fungamwango

KILA miaka inavyozidi kwenda mbele, ndivyo teknolojia inavyozidi kurahisisha maisha. Hivi sasa kila kitu kinapatikana dukani kikiwa tayari kimeshakobolewa au kusagwa, tena kwa bei rahisi tu. Unaweza kupimiwa au ukakuta tayari imefungwa kwenye mifuko. Unga na nafaka zingine na kukobolewa zinanunuliwa zikiwa tayari tofauti na zamani.

Kwa sasa niseme tu hata tui la nazi linauzwa madukani, wakati zamani ni lazima nazi ikunwe kwenye kibao cha mbuzi. Nimeona kwenye soko moja Dar es Salaam, kabichi ikiwa tayari imekatwakatwa na kufungwa kwenye kifungashio ikiuzwa wakati ninavyojua ilikuwa inanunuliwa nzima na mnunuaji atalazimika akaikatie nyumbani.

Nakumbuka kinamama zamani walikuwa wanatwanga kisamvu kwenye kinu baada ya kukinunua sokoni lakini siku hizi wananunua kikiwa kimetwangwa tayari. Haya ni maendeleo ingawa kuna watu wanasema imewafanya baadhi ya kinadada zetu kuwa wavivu.

Miaka ya nyuma iwe mijini au vijijini, ilikuwa ngumu mno kupata moja kwa moja unga wowote ule ukiwa umesagwa. Huko vijijini ndiyo kabisa kwa sababu mahindi yakishavunwa yanawekwa kwenye vichanja vya kuhifadhia chakula halafu taratibu yanakwenda kusagwa ili upatikane unga pale inapohitajika. Ukimalizika watu wanakwenda mashineni tena.

Zamani sana enzi wa mababu zetu, walikuwa wanasaga kwa kutumia mawe makubwa mazito. Lakini baadaye ikaja teknolojia ya mahine za kusaga na baadaye kukoboa. Kwa hiyo mtu alikuwa na hiari yake, asage moja kwa moja au akoboe na kusaga.

Hapo ndipo zilipoanza kuingia mashine za kusaga zinazotumia dizeli hasa vijijini. Hadi leo baadhi ya vijiji kwenye mikoa mbalimbali bado zipo. Kwenye miji mikubwa ikiwamo Dar es Salaam, Arusha, Moshi na Tanga baadhi ya sehemu kulikuwa na mashine za kukoboa na kusaga zinazotumia umeme.

Sasa shughuli inaanzia hapa. Kuna baadhi ya vijiji vilikuwa karibu na mashine. Maana wakati huo unaweza kukuta vijiji kumi, lakini kuna mashine moja tu na iko mbali sana na vijiji vingine. Wengine ni saa nzima au masaa mawili kwa miguu kutoka kwao kwenda kwenye mashine.

Sasa kuna familia zenye watoto ambao umri wao wameshaanza kuendesha basikeli, au vijana, watatumwa kwenda mashineni. Watafungashiwa mzigo na kufunga nyuma ya basikeli. Inakuwa ni shughuli ya siku nzima.

Kuna vijiji ambavyo vilikuwa mbali sana na mashine. Walikuwa wakiondoka jioni na kwenda kulala kwenye mashine ili kuwahi foleni. Kama si hivyo, basi atakayepewa jukumu la kwenda kusaga atatakiwa kudamka alfajiri na mapema ili kuwahi foleni.

Kama nilivyosema ni kazi ambayo kwa watoto na vijana wakati huo kwa sababu ilikuwa ni ya kutwa nzima, wakati mwingine baadhi walikuwa wakikataa kwenda. Kwa sababu hawatocheza, wala kufanya kitu kingine wanachokipenda kwa siku hiyo.

Hapo ndipo wazazi wanajitokeza na kumpiga mkwara yoyote aliyetumwa kwenda mashineni akakataa kuwa hatopata chakula. Na kwa sababu wazazi wa zamani walikuwa hawatanii, hawataniwi na walikuwa wanasimamia kile ambacho wanachokisema na kukiamini, basi kijana anajua kabisa hatokula nyumbani hadi chakula hicho kama kitaenda kusagwa na mtu mwingine kimalizike. Atakula kwa mjomba, shangazi sawa, lakini nyumbani hali, hadi pale jambo hilo litakapowekwa sawa au kuomba msamaha.

Kwa upande wa kinadada na kinamama nao walikuwa na vinu vyao ambavyo walikuwa wanatumia kutwanga mahindi. Hayo yalitumika kwa ajili ya kande na aina nyingine ya mapishi. Walitwanga pia mpunga kama haukuwa mwingi sana wa kupeleka mashine. Kisamvu nacho pia kilitwangwa.

Kinamama walitumia njia hii pia kuwafundisha mabinti zao kutwanga ili wasije kuaibika baadaye watakapoolewa na anayejifanya kukataa, atapata adhabu ya kutokula mlo wa siku ile.

Kilichofurahisha wakati huo ni upendo. Anayetwanga hatotwanga peke yake. Wakipita kinamama wakimuona mwenzao wanafanya kazi hiyo watamsaidia hata kwa dakika tano. Ili mradi tu kumfanya amalize kazi ile kwa muda mfupi. Hata majirani nao wakati huo. Wakimuona mwenzao anatwanga na wao watasogea kumsaidia.

Ilifurahisha na kuwa burudani kuona akinamama watatu au wanne wakiwa pamoja, kila mmoja akiwa na mchi wake, wakitwanga kwa pamoja. Wawili wakipeleka chini, wawili wanainua juu.

Wengine walikuwa wakitwanga kwa mbwembwe, anarudisha mchi juu, anauachia, halafu anaudaka tena kabla ya kutwanga. Wakati mwingine huku wanaimba.

HADITHI

MILIO mitatu ya risasi ilisikika maeneo ya Keko Bora, Dar es Salaam. Sauti hizo za risasi ziliwafanya watu kutimua mbio na kutafuta chaka la kujificha. Kila mmoja alidhani ni majambazi waliovamia kwa ajili ya kupora pesa dukani au kwenye vibanda vya mawakala wa kampuni za simu.

Haikuwa hivyo. Aliyedhaniwa kuwa ni jambazi alichofanya ni kumpora mwanamke mtoto mwenye umri wa mwaka mmoja tu na kuondoka naye akiwa kwenye gari aina ya Toyota IST. Huyu jamaa aliyefanya hivyo ni nani? Ni kwa nini alimteka mtoto? Mtoto ni wa nani? Mwanamke aliyeporwa mtoto anamfahamu mporaji? Fuatilia kisa hiki kitamu, cha kusisimua na kuhuzunisha.

# Nina Jambo Langu-14

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**



"Habari za siku nyingi shemeji zangu, wifi zangu na wakwe zangu. Samahani sana, mimi nimekuja hapa kama mgeni tu mwalikwa. Sikuja kama mwanandugu. Hapa mimi nimekuja kwa nia tu ya kumtetea rafiki yangu au shoga yangu Neema au mama Diana.

"Ukweli ni kwamba aliyemteka mtoto wenu Diana wala si hawara yake kama wengi mlivyokuwa mnadhani. Aliyemtemka ni rafiki ya mjomba wangu. Jina siwezi kuwatajia na hii ni baada ya kusimuliwa kisa kizima nilichofanyiwa na Ben. Nia haikuwa mbaya.

"Nitawaambieni tu. Wote mnafahamu hapa kuwa Ben ndiye mume wangu ambaye alinioa kwa ndoa kanisani na wengi wenu hapa mlihudhuria. Alichonifanya Benson ilikuwa baada ya kumzaa Tina tu, akaanza kutoonekana nyumbani, kulala nje, kurudi usiku na siku isiyo na jina akaondoka moja kwa moja."

Maelezo yale yalionekana kuwaingia wote waliokuwa kwenye mkutano huo.

Wote wanachofahamu hapo ni kwamba Ben alitengana na mzazi mwenzake kwa sababu alimfumania ndani na mwanamume mwingine. Tena waliambiwa walikuwa wanafanya hivyo, wakati mtoto bado mchanga kabisa, kitu kilichowakasirisha ndugu wote.

Ndivyo Ben alivyowadanganya ndugu zake, akamkimbia Ester kwenda kuishi kwingine. Zote hizo zilikuwa kutafuta sababu. Tayari alishampata mwanamke mwingine Neema. Kukacha kurudi nyumbani au kuchelewa, alikuwa anakwenda kwa Neema alikompangia. Akaionja asali akataka kuchonga mzinga.

Akamtengenezea hilo zengwe la kumfumania ili kupata uhalali kutoka kwa ndugu zake, akahamia moja kwa moja kwa Neema na kumtelekeza kabisa Ester akiwa na mtoto mchanga. Wakafunga ndoa ya Kiserikali na Neema.

"Labda kuna kitu aliwadanganya. Ukweli ni kwamba alinitelekeza nikiwa na mtoto mchanga Tina na kwenda kuona mwanamke mwingine." Alisema na kuwaangalia jinsi watu walivyokuwa wakisikiliza kwa makini, wakiwa kama hawaamini kile alichokuwa anaongea.

"Iliniuma sana. Nilikuwa simjui mwanamke huyo ni nani. Kumbe ni huyu hapa aliyenialika, Neema." Ester alinyamaza na kukohoa kidogo, akiwaacha wahudhuriaji waendelee kutafakari.

"Nilichanganyikiwa hadi mjomba wangu akaamua kunichukua kwake Ubungo. Na kwa hasira akataka alipize kisasi. Ana rafiki yake mmoja hivi ambaye alimpa kazi ya kupeleleza na akajua Ben yuko wapi. Akajua kuwa ameoa na ana mtoto. Wazo lao na mjomba ilikuwa kumteka mtoto ili baadaye kumpigia simu amfuate mtoto na atakapofika ndipo wakae naye na kumuuliza sababu ya kunitelekeza na kwa nini amhudumii mtoto. Ndipo kijana yule rafiki yake kaka akafanya kazi hiyo ya kumteka mtoto wenu huyu.

Kwa bahati mbaya sana namba za Ben za simu zilikuwa zimebadilika. Zile ambazo nazifahamu hazikuwa hizo. Alikuwa amesajili laini zingine ambazo mimi sizifahamu. Wazo likaja lingine kumteka yeye. Hilo mimi nikapinga. Nikawaambia kama imeshindikana basi tu itafutwe namna mtoto arudishwe."

Maneno hayo yaliwashangaza wote ndani. Kumbe mke wa Ben ambaye alifunga naye ndoa, Ester ndiye chanzo cha mtoto Diana kutekwa. Na ametekwa kwa sababu tu Ben alimtelekeza mtoto mwingine Tina bila matunzo.

Lengo halikuwa baya kama walivyodhani. Ilikuwa baada ya hapo apigiwe simu tu baba mtu aende alipo mtoto ndiyo akutane na mkewe Ester na familia yake, ili kuangalia mustakabali wa mke na mtoto.

"Iliposhindikana kumpata bwana huyu, tukawa tunajiuliza sasa tutamrudisha vipi, ndipo nilipokutana na watu ambao waliniunganisha na huyu dada na tulipokuwa tunaongea, tukajikuta wote sisi ndiyo wenye mkasa huu. Mimi ndiye niliyetelekezwa na mtoto na yeye ndiye mtoto wake alitekwa. Nikamchukua na kwenda kumkabidhi mtoto wake nyumbani kwangu." Ester akazidi kupasua.

"Mimi sina ugomvi na huyu dada, japo Ben aliniacha mimi na kwenda kumuoa kwa ndoa ya Kiserikali, ndiyo maana wote wawili tukaungana ili kuikomesha hali hii ya kudhalilisha wanawake.

"Wanawake tunafanywa kama buyu la asali. Mtu anachovya hapa, halafu akichoka anaacha anakwenda kuchovya kwingine. Leo nimekuja hapa kumtetea shoga yangu kuwa wala hana hawara wala nini ni mimi niliyetelekezwa, ndiye niliyesababisha mtoto wenu atekwe na siyo kama nina mpango tena wa kutaka kuendelea kuishi naye.

"Mimi nina uwezo wa kuendesha maisha yangu bila yeye. Siwezi kurudiana naye. Mtoto wenu Tina yupo nyumbani na ana afya tele."

Kimya kilitawala. Kila mmoja alikuwa akivuta picha tukio lile lilivyotokea. Kumbe mke wa zamani wa Ben ndiye aliyesababisha hayo kisa Ben alimtelekeza. Neema aliingia kwenye mzozo mkubwa kutokana na uamuzi ya Ester. Akaambiwa kahaba. Hawara yake ndiye aliyemteka mtoto.

Ben tayari alikuwa amempa talaka Neema. Kumbe ilitolewa kimakosa. Ester tayari ameshasema kuwa hana tena mpango wa kurudiana na Ben. Neema naye ana talaka mkononi.

Lilikuwa pigo kubwa kwa Ben. Tayari alishaanza kuona makosa yake. Papara, hasira na wivu vilimponza. Angesubiri kidogo asingetoa talaka kwa pupa. Kumtuhumu mkewe Neema kuwa huenda alikuwa na mwanamume nje ambaye alimteka mtoto lilikuwa kosa kubwa.

"Nashukuru sana shoga'angu Ester. Mimi nimekuita hapa kwa lengo moja tu. Uthibitishe kuwa mtoto hakutekwa kwa hawara yangu. Kumbe mtoto ametekwa si kwa sababu yangu, ila kwa sababu ya Ben. Hakuwahi hata siku moja kuniambia kuwa alikuwa na mke, tena alimuoa kwa ndoa." Sasa ilikuwa zamu ya Neema kuielezea familia nini kimetokea na mtazamo wake.

Ben hakuona kama anaweza kuokoa chochote pale. Tayari aliona ameshakosa mwana na maji ya moto. Ester na Neema wameungana. Walipoungana yeye hapajui. "Walionana wapi hawa?" Alijiuliza.

Alimuoa Ester. Akamtelekeza. Ni kutokana na penzi jipya la Neema. Lakini kwa kilichotokea aliona kabisa yupo karibu kukosa mwana na maji ya moto.

**INAENDELEA JUMAPILI**

# BONGO FLEVA WAMLILIA JPM KWA NYIMBO



WASANII wa muziki wa Bongo Fleva, wanaendelea kuomboleza kifo cha Rais Dk. John Magufuli, kwa kutoa nyimbo mbalimbali za majonzi

Wasanii wa hivi karibuni waliotoa nyimbo zao ni Diamond Platnumz akiwashirikisha wanamuziki kutoka lebo ya WCB, Enock Bella akishirikiana na wasanii wengine wanaounda kundi la Tanzania Artist na Kala Jeremiah.

Aidha, wengine waliojitokeza kutunga nyimbo ni Mrisho Mpoto, Ommy Dimpoz, Peter Msechu na Tanzania All Stars.

## Pili Kitimtim hakutimiza ndoto kwa Magufuli

MSANII wa vichekesho, Pili Kitimtim, amesema ndoto yake ya kumshirikisha Rais Dk. John Magufuli, katika sanaa ya jukwaani umekatika baada ya kifo chake cha ghafla.

Amesema tofauti na viongozi wengine, Rais Magufuli alikuwa karibu na wasanii wa aina zote, hivyo alikuwa na wazo la kuandaa shoo ya jukwaani na kumwalika kiongozi huyo ili kuona vipaji vya wasanii wake.

"Nilikuwa nataka kuwashirikisha wezangu kuandaa shoo ya jukwaani na kumualika Magufuli ili aangalie vipaji vyetu, hakuwa mbaguzi alitushika mkono kila mtu kwa kweli hatujui wapi tunakwenda," amesema.



## Bongo Muvi wajipanga kwenda Chato

WASANII wa Bongo Muvi, kesho wataanza safari ya kwenda katika mazishi ya aliyekuwa Rais wa Tanzania, John Magufuli yatakayofanyika Chato Mkoa wa Geita.

Steve Nyerere ameliambia gazeti hili kuwa wasanii hao wataanza safari hiyo saa 12 asubuhi.

"Alikuwa kama baba yetu, kwetu sisi wasanii wa filamu tunamuona Magufuli kama mwanamapinduzi halisi wa nchi na katika tasnia alifanya iaminike sasa tunafaidika." Amesema Steve.



# TeamViewer yajitosa kuidhamini Man United

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United imeingia makubaliano na Kampuni ya TeamViewer kwa ajili ya udhamini wenye thamani ya pauni milioni 235 huku mkataba wao na Chevrolet ukielekea mwishoni.

Dili hilo ambalo ndiyo udhamini mkubwa zaidi kwenye Ligi Kuu England, itashuhudia nembo ya TeamViewer ambayo itakuwa na rangi nyeupe itakaa mbele kwenye jezi za United mwanzoni mwa msimu ujao.

Chevrolet wamekuwa wadhamini wakuu wa jezi za United karibu miaka saba licha ya kuongeza makubaliano ya miezi sita, ambayo itawepeleka mpaka nusu ya msimu ujao na hakuna mpango wowote wa kuongeza mpaka miaka nane.

TeamViewer ni Kampuni ya Ujerumani inayojihusisha na masuala ya teknolojia iliyoanzisha mwaka 2005.

United waliamua kushirikiana na TeamViewer baada ya kuona wanafaa kwa sababu wana nguvu na wanamvuto katika kupanua soko la kimataifa.







# MOURINHO MAMBO MAGUMU SPURS

**LONDON,** England

MAMBO yanaonekana kuwa magumu kwa kocha wa Tottenham Hotspur, Jose Mourinho, baada ya kushindwa kukiongoza kikosi hicho kufuzu robo fainali ya Ligi ya Europa.

Totternham Spurs ilikubali kichapo cha mabao 3-0 kutoka kwa Dinamo Zagreb ya Croatia katika mechi ya mkondo wa pili, iliyolazimika kwenda kwenye muda wa nyongeza baada ya dakika 90 kumalizika kwa wenyeji kushinda 2-0, na hivyo kufanya kuwa sare ya 2-2 kufuatia mchezo wa kwanza Spurs ilishinda 2-0.

Baada ya matokeo hayo, mashabiki mbalimbali wameonekana kumnyooshea kidole Mourinho wakimtaka mmiliki wake, Daniel Levy kumtimua kwa kuwa hawaoni umuhimu wowote wa kuendelea naye wakiamini zama zake zimefika mwisho.

Hoja ya mashabiki imekuja baada ya kutathimini mwenendo wa timu hiyo tangu Mourinho alivyoichukua timu hivyo Novemba, mwaka 2019, ushiriki wa ligi na vikombe mbalimbali ikiwamo cha Ligi ya Europa ambapo wametolewa usiku wa kuamkia jana.

Katika msimamo wa Ligi Kuu England, Spurs iko katika nafasi ya nane ikiwa na alama 45 na kuzua hofu ya kufuzu katika Ligi ya Mabingwa Ulaya. Mourinho ni miongoni mwa makocha bora duniani ambao wamepata mafanikio makubwa ikiwamo kutwaa Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya mara mbili akiwa na vilabu vya FC Porto na Inter Milan na pia ubingwa wa ligi kwa baadhi ya timu alizozifundisha kama Porto, Chelsea, Inter Milan na Real Madrid.

Kwa mwenendo anaokwenda nao katika timu ya Totternham unaashiria kutofikia mafanikio hayo ya nyuma.

# *Carragher awatoa Salah, Kane sokoni*

**MADRID,** Hispania

MLINZI wa zamani wa Liverpool, Jamie Carragher, amesema anaamini ofa za wachezaji Mohamed Salah na Harry Kane hazipo tena kutoka katika klabu za Barcelona na Real Madrid.

Kumekuwa na uvumi katika wiki za hivi karibuni kuwa Salah hafurahii kuwapo Liverpool, wakati msimu mwingine wa kumaliza pasipo kombe unaweza kumfanya Kane aangalie hatima yake kule Tottenham Hotspur.

Lakini, Carragher haoni kama Real Madrid na Barcelona wanaweza kutoa fedha nyingi kumsajili Salah au Kane.


"Salah na Kane wameshaachwa na boti ya kujiunga na Real Madrid au Barcelona,"amesema Carragher akinukuliwa na Sky Sport.

"Kwa wachezaji hao wote wawili, nadhani unazungumza pauni milioni 120 pamoja, labda zaidi, na sidhani kama mtu yeyote atatumia fedha nyingi kwa wachezaji wa umri huo sasa" aliongeza.






# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# HAZARD APITIA WAKATI MGUMU

Kuhusiana na hatima ya kuendelea kucheza soka endapo atafanyiwa operesheni nyingine ya...

**MADRID,** Hispania

DAKTARI ameonya kiungo fundi wa Real Madrid, Eden Hazard, huenda asicheze tena kandanda iwapo atafanyiwa upasuaji mwingine wa kifundo cha mguu.

**Raia huyo wa Ubelgiji amekuwa akisumbuliwa na majeraha tangu ajiunge na Real Madrid akitokea Chelsea kwa mkataba wenye thamani ya pauni milioni 130 hapo mwaka 2019.**

Amewekwa pembeni na shida nyingine ya kifundo cha mguu kwa sasa na inaeleweka anataka operesheni nyingine.

Lakini daktari, Jose Gonzalez, ambaye anafanya kazi kwa wapinzani wa Real, Atletico Madrid, ameonya kuwa operesheni ya tatu ya kifundo cha mguu inaweza kumaliza kazi ya Hazard kucheza tena soka.

Amenukuliwa na gazeti la Ondacero akisema: "Hazard lazima afanye mazoezi magumu na timu kwa muda mrefu.

"Kwa uzoefu wangu ni ngumu kwake kurudi kucheza kwenye kiwango chake na Real Madrid msimu huu.

"Ikiwa mchezaji anarudi baada ya kuumia kwa muda mrefu bila kupata mazoezi magumu, jambo la kawaida kuona kuwa anacheza kwa woga akiogopa kuumia tena.

"Ana wasiwasi, anataka kuonyesha kuwa ana thamani na anataka kutoa asilimia 100 na hayupo katika hali hiyo.

"Operesheni ya tatu kwenye kifundo cha mguu cha Eden Hazard ni hatari sana, kuna uwezekano wa kumfanya asicheze tena soka.

Alirudi tu hivi karibuni katika ushindi wa Jumamosi wa 2-1 dhidi ya Elche na kocha wake, Zinedine Zidane alisema "hawezi kuelezea" kwa nini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 alipata shida nyingine.

Real Madrid ingependa kuahirisha upasuaji, lakini Ubelgiji inahamu ya Hazard kushughulikiwa kumaliza majeruhi yake haraka ili aweze kurudi katika hali yake ya kawaida kwa ajili ya michuano ya Mataifa ya Ulaya itakayochezwa Juni mwaka huu.

## ZISIKUPITE

### HAALAND AZIDI KUWINDWA

REAL Madrid na Barcelona zote zipo tayari kutoa changamoto kwa Manchester City, Manchester United na Chelsea katika mbio za kumsajili nyota wa Borussia Dortmund na Norway, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 20. ***(AS)***

### HAALAND: NITAONDOKA

STRAIKA wa Timu ya Taifa ya Norway, Erling Haaland, anataka kuondoka Dortmund kipindi kinachokuja cha majira ya joto huku akitajwa kutaka kwenda Real Madrid. ***(ABC)***

### MORIBA ANUKIA UNITED

MANCHESTER United inafikiria kumsajili kinda wa Barcelona mzaliwa wa Guinea, mwenye umri wa miaka 18, Ilaix Moriba. ***(Mundo Deportivo)***

### MBAPPE KUPEWA MKATABA

KLABU ya Paris St-Germain ipo tayari kutoa ofa ya mkataba mpya kwa straika wake, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 22, ambaye ana thamani ya euro milioni 30, huku akiwa pia anawaniwa na Real Madrid pamoja na Liverpool. ***(L'Equipe via Mirror)***

### BARCA YAMTAKA AGUERO

NYOTA wa Manchester City na Argentina, Sergio Aguero mwenye umri wa miaka 32, na kiungo wa Liverpool, Georginio Wijnaldum mwenye umri wa miaka 30, wapo kwenye orodha ya kuwaniwa na Barcelona. ***(AS via Sport Witness)***

### JUVE YAMGANDA POGBA

JUVENTUS inaendelea kumfuatilia kiungo wa Manchester United, Paul Pogba, huku mkataba wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa ukitarajiwa kumalizika ifikapo Juni mwakani. ***(Calciomercato)***

### UNITED, POGBA BADO

MANCHESTER United bado haijatoa ofa ya mkataba mpya kwa kiungo wake, Paul Pogba licha ya kutajwa kwamba anataka kuondoka. ***(Telegraph - subscription required)***

### MOURINHO KUTAJIRIKA

KAMA Tottenham Spurs itamfukuza kocha wake, Jose Mourinho watalazimika kumlipa pauni milioni 25. ***(Mirror)***

### BAILLY NJIA MOJA

MLINZI wa Ivory Coast, Eric Bailly mwenye umri wa miaka 26, atakaa ofa ya mkataba mpya wa kuendelea kuitumikia Manchester United kwa sababu hana nafasi kwenye kikosi cha kwanza. ***(Sun)***

### OLSEN KURUDI ROMA

GOLIKIPA wa Sweden, Robin Olsen mwenye umri wa miaka 31, hataongeza mkataba wa mkopo na Everton kwa sababu anajipanga kurejea katika klabu yake ya zamani ya AS Roma ifikapo mwishoni mwa msimu huu. ***(Mail)***

HABARI MICHEZO

# Ihefu FC kurejea kibabe Ligi Kuu

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Ihefu FC umeandaa mikakati kuhakikisha inafanya vizuri katika mechi zao 10 zilizobakia ili kuendelea kubakia katika msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, imefahamika.

Katibu Mkuu wa Ihefu FC, Fred Chalamila, alisema wanatambua wako katika majonzi ya msiba wa aliyekuwa Rais wa Tanzania Hayati Dk. John Pombe Magufuli (pichani chini), lakini wanapambana kutumia mapumziko yaliyotolewa kuimarisha kikosi chao.

Chalamila alisema awali wakati ligi imesimama kupisha kalenda ya kimataifa, timu yao iliendelea na programu za mazoezi ili kukiimarisha zaidi kikosi chao kuelekea mechi ngumu zilizobakia.

"Tuko katika wakati mgumu kwenye msimamo wa ligi, ndio maana hatujavunja kambi, hivyo tunahitaji kupambana katika kuhakikisha tunatumia vyema hizi siku za mapumziko kwa benchi letu la ufundi linaloongozwa na Zuberi Katwila kufanyia kazi upungufu wetu kwa ajili ya mechi zijazo," alisema Chalamila.

Aliongeza bado hawajakata tamaa na wataendelea kupambana kuhakikisha kikosi chao kinafanya vizuri katika michezo 10 na hatimaye ndoto ya kubakia Ligi Kuu Tanzania Bara inatimia.

Naye Katwila alisema licha ya jukumu la kurekebisha upungufu alionalo hasa katika safu ya ushambuliaji, ana imani wachezaji wake wamebadilika na kila mmoja anaonyesha kiu ya kupata matokeo chanya.

"Nina imani na wachezaji wangu kufanya vizuri, ukiangalia mechi yetu ya mwisho dhidi ya Azam FC, walicheza vizuri ila tulishindwa kutumia nafasi tulizotengeneza pamoja na mabeki wetu kutokuwa makini jambo ambalo tumeshaliboresha kwa sasa," alisema Katwila.

Aliongeza haoni timu hiyo ikishuka daraja kwa sababu inaonyesha ushindani katika kila mechi tofauti na ilivyokuwa katika mzunguko wa kwanza.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Ihefu FC yenye pointi 20 sawa na Mbeya City iko kwenye nafasi ya 17 baada ya kucheza michezo 24 huku Mwadui FC ya Shinyanga yenye pointi 17 ikiburuza mkia.



# ZULFA, HALIMA VUNJABEI WAMLILIA RAIS MAGUFULI

**Na Saada Akida**

MABONDIA wa ngumi za kulipwa wanawake wa hapa nchini, Zulfa Macho na Halima Vunjabei wameguswa na msiba wa aliyekuwa Rais wa Tanzania, Dk. John Pombe Magufuli na kusema kiongozi huyo atakumbukwa zaidi na wanamichezo kutokana na kuhamasisha ushindi.

**Wakizungumza na gazeti hili kwa nyakati tofauti baada ya pambano lao la kusaka Malkia wa Ulingo lililotarajiwa kufanyika Machi 27, mwaka huu kuahirishwa, mabondia hao walisema msiba huu uliotokea ni pigo kwa Watanzania.**

Zulfa ambaye ni mtoto wa kiungo wa zamani wa Simba na Timu ya Taifa (Taifa Stars), alisema jambo lililopangwa na Mungu binadamu hawezi kuliepuka lakini aliweka wazo bado Watanzania walikuwa wanamhitaji kiongozi huyo.

"Watanzania kila kona wanalia kwa sababu kikubwa wanakumbuka mambo mazuri aliyoyafanya," alisema Zulfa.

Kuhusu kusogezwa mbele kwa pambano dhidi ya Vunjabei, bondia huyo alisema licha ya kuwa katika kipindi cha maombolezo, ataendelea na mazoezi ili kuuweka mwili wake tayari.

"Nitaendelea kujifua ili kuhakikisha kipigo nilichokiandaa kinakamilika na Watanzania waone burudani, burudani ya raundi 10 lazima ipatikane, namweleza afahamu kipigo kitamhusu Halima, acha tumalize kwanza msiba," alisema Zulfa.

Naye Vunjabei alisema maombolezo yake yataambatana na mazoezi makali kwa sababu anataka kumuenzi Rais Magufuli kwa kutoa kichapo.

"Mimi binafsi ninataka kumwenzi Magufuli, Baba na Jemedari kwa kuhakikisha ninashinda mechi na si vinginevyo," alisema bondia huyo.

Hata hivyo bondia huyo alimpongeza Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuapishwa kuwa Rais wa kwanza mwanamke na kuongeza anahitaji kupewa ushirikiano ili kukamilisha mipango yote mizuri ya kuendeleza nchi.

Mabondia wengine watakaopigana siku hiyo ni pamoja na Fatuma Yazidu dhidi ya Dorothea Muhoza wakati Happy Daudi ataonyeshana kazi dhidi ya Leila Yazidu huku Lulu Kayage atazipiga na Jesca Mfinanga, Mwanne Haji atapambana na Sarafina Julius, Agnes Kayange atacheza dhidi ya Mwajuma Pengo, Grace Mwakamele vs Asha Gota wakati Salma Kihombwa atapimana udabu dhidi ya Mariam Mungi na Zawadi Kutaka atazidunda na Martha Kimaro.



Makocha wasaidizi wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Juma Mgunda (kulia) na Suleiman Matola, wakibadilishana mawazo kwenye mazoezi ya timu hiyo inayojiandaa na mechi za kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa Afrika (AFCON), dhidi ya Equatorial Guinea na Libya. **PICHA: TFF**

# *Msiba wa JPM waibadilisha Simba SC*

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imetangaza kubadilisha mwonekano wa picha zake kwenye akaunti zake za mitandao ya kijamii kuwa za rangi nyeupe na nyeusi kwa siku 21 ili kumwenzi Dk. John Magufuli, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Barbara Gonzalez amendika kwenye mtandao wake wa kijamii wameamua kufanya hivyo ili kuenzi mema ambayo aliwafanyia Wanasimba na Watanzania kwa jumla.

Hata hivyo amesema rangi imebadilika, isipokuwa sehemu zenye rangi nyekundu tu ndizo zitakuwa hazina mabadiliko.

"Katika kuomboleza kifo cha mpendwa wetu, Rais Dk. John Magufuli, tumeamua kubadili mwonekano wa picha zetu kwenye mitandao ya kijamii ya klabu kuwa nyeusi na nyeupe, isipokuwa sehemu zenye rangi nyekundu. Klabu ya Simba tunaendelea kumwombea kwa Mwenyezi Mungu aipumzishe roho yake mahala pema peponi." Aliandika Barbara kwenye mtandao wake wa kijamii.

Wakati huo huo Simba imekuwa moja kati ya timu tano ambazo hazijapoteza mechi yoyote ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Simba ambayo haijaruhusu bao lolote, ikiwa pamoja na Wydad Casablanca ya Morocco, haijapoteza mchezo wowote ikiwa ni moja kati ya timu tano, kati ya 16 zinazoshiriki hatua ya makundi msimu huu.

Timu zingine ambazo hazijapoteza mechi ni Wydad Casablanca, Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini, Esperance ya Tunisia na MC

# Michezo

Jumapili Machi 21, 2021

Nipashe





Hazard apitia wakati mgumu

UKURASA 22



Rais wa Shirikisho la Soka Nchini (TFF), Wallace Karia, akiweka saini katika kitabu cha waombelezaji kufuatia kifo cha aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Pombe Magufuli, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MTANDAO**

## Simanzi wadau wakimuaga JPM

**Na Waandishi Wetu**

HALI ya vilio, simanzi, na majonzi ilionekana kutawala kutoka wa wadau wa michezo na wasanii mbalimbali walipojitokeza kuuaga mwili wa aliyekuwa Rais wa Tanzania, Dk. John Pombe Magufuli kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana.

Viongozi wa Shirikisho la Soka Nchini (TFF) wenyewe walituma wawakilishi kuanzia kwenye ibada maalumu iliyofanyika jana asubuhi kwenye Kanisa la Mtakatifu Petro lililopo Oysterbay jijini huku mwanamuziki, Harmonize akitokwa na machozi.

Mwekezaji na Mwenyeiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, Mohamed Dewji 'Mo' alikuwa mmoja wa wanamichezo waliofika kwenye Uwanja wa Uhuru kutoa heshima za mwisho kiongozi huyo aliyefariki dunia Machi 17, mwaka huu.

"Naungana na Watanzania wenzangu katika Uwanja wa Uhuru asubuhi hii kutoa heshima zangu za mwisho kwa mpendwa wetu Hayati Rais Dk. John Magufuli. Nenda salama Dk. Magufuli. Upumzike kwa amani." Mo alisema.

Chama cha Netiboli Tanzania (Chaneta), chenyewe kiliwakilishwa na wajumbe wote wa Kamati ya Utendaji katika mchakato huo wakiongozwa na mwenyekiti wao, Devotha Marwa.

Rais Magufuli anatarajiwa kuzikwa nyumbani kwao Chato Machi 26, mwaka huu na leo wananchi wa Dar es Salaam wataendelea kutoa heshima zao za mwisho.

# *Mwambusi kurejesha dozi Yanga*

**Na Saada Akida**

### Afunguka ndiyo njia pekee itakayowaimarisha katika vita vya kuwania ubingwa...

LICHA ya kuwa kwenye kipindi cha maombolezo ya msiba wa aliyekuwa Rais wa Tanzania, Dk. John Pombe Magufuli, Kaimu Kocha Mkuu wa Yanga, Juma Mwambusi amesema anakiandaa kikosi chake kutoa ushindi mnono katika kila mechi ya Ligi Kuu Bara na mashindano ya Kombe la FA watakayocheza.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Mwambusi alisema ameandaa programu maalumu kwa wachezaji alionao sasa na nyingine ambayo itakuwa ya awamu ya pili baada ya wenzao walioko katika Timu ya Taifa (Taifa Stars), watakaporejea.**

Mwambusi alisema kitu kikubwa ambacho anakifanyia kazi ni kuongeza makali kwenye safu ya ushambuliaji ambayo ndiyo yenye msingi wa kuvuna pointi tatu.

Kocha huyo alisema anataka kuona timu yake inamaliza 'mechi' mapema kwa kufunga mabao mengi na anaamini hali hiyo itawaondolea presha wachezaji kwenye dakika za mwisho za mchezo.

"Nafahamu nchi iko katika wakati mgumu baada ya kupata pigo kubwa la kuondokewa na Rais Magufuli ambaye alikuwa na mchango mkubwa katika sekta ya michezo, lakini sisi pia tuko kwenye vita kubwa ya kuwania ubingwa, mabao ndio yatatufanya kufikia malengo, tunajua ligi ikirejea, kila timu itaingia kivingine," alisema Mwambusi.

Aliongeza kwa muda wa wiki moja ambao amesimamia timu hiyo, amebaini kikosi kimebadilika na wachezaji wote wanazungumza 'lugha' moja ya kupambana kusaka matokeo mazuri.

"Kwa sasa ni mapema sana kuweka wazi moja kwa moja mbinu za kiufundi tunazozifanyia kazi kwa sababu nina wachezaji pungufu, kikubwa ninaendelea kufanyia kazi upungufu nilioubaini, ninaangalia pia utimamu wa mwili kwa mchezaji mmoja mmoja, halafu baadaye tutajenga mfumo tutakaoutumia, nina hakika tutafanikiwa," Mwambusi alisema.

Aliongeza benchi la ufundi na wachezaji wote wa Yanga wako tayari kukabiliana na ushindani na sasa kwao kila mechi ni sawa na fainali na amewataka mashabiki na wanachama wa timu hiyo kuendeleza mshikamano.

"Baada ya hapo nitatengeneza muunganiko wa jumla, lakini pia suala la umaliziaji limekuwa tatizo, tunachotakiwa ni kuongeza umakini kwa nafasi tunazotengeneza uwanjani, tunapoteza nafasi nyingi, hili si jambo zuri, ukipata mpinzani imara anakumaliza kwa kutumia nafasi yake moja au mbili anazozitengeneza," alisema Mwambusi.

Aliweka wazi timu yake kwa sasa inafanya mazoezi kwa vipindi viwili kwa siku ili kuimarisha stamina lakini atakapoona wamefikia kiwango anachokihitaji, idadi ya programu za mazoezi ya uwanjani zitapungua na ataelekea kwenye darasa la kutumia picha za video.

"Tunataka tuwe imara kila idara ili ligi itakapoanza tena tuwe na uhakika wa kupata pointi tatu kwa kila mechi tutakayocheza bila kujali jina la mpinzani, ingawa tunaamini hakuna mechi ndogo kwa sababu kila timu inaingia uwanjani na malengo yake," Mwambusi alisema.

Aliongeza mazoezi yake ameyagawa katika awamu mbili kwa sababu akili yao pia imejielekeza katika kuwania taji la Kombe la FA ambalo mechi zake huchezwa kwa mtindo wa mtoano.

"Kuna FA, mechi hizi hazihitaji sare, ni lazima pia kama mwalimu uandae mikakati ya kumaliza mechi na ushindi, kubadilisha mbinu haraka baada ya kufahamu ubora wa mpinzani wako, hatutaki kurudia makosa ya msimu uliopita, tunahitaji heshima na furaha msimu huu," aliongeza kocha huyo wa zamani wa Mbeya City.

Yanga yenye pointi 50 ndio vinara wa ligi hiyo baada ya kucheza mechi 20 wakati katika mechi ya hatua ya robo fainali ya Kombe la FA itasafiri kwenda Sumbawanga kuwafuata wenyeji wao Tanzania Prisons, katika tarehe mpya itakayotangazwa.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >